
Haliuzwi
MACHI 28, 2026
/islamicftz
Ramadhan 20 1447
# IMAAN
ISSN 5618 - NO. 574
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah



## Mageuzi EAC yaamsha matumaini mapya ya ushirikiano

# Mwinyi aongoza maelfu futari ya kitaifa Zanzibar





■ Watu 27,345 walishiriki tukio hilo, kwa mujibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar (OCGS), wanaume wakiwa 18,771 na wanawake wakiwa 8,574

## Mufti akemea wanaotumia dini kuvuruga amani

يا أيها الذين آمنوا كتب عليكم الصيام كما كتب على الذين من قبلكم

## Rais UAE aonya Iran: Falme za Kiarabu si mawindo rahisi



## Dkt. Mwigulu: Kuhifadhi Qur'an kuendane na kuiishi kivitendo

## Iran, Marekani wachochea makali bei ya mafuta






Rais wa Falme za Kiarabu (UAE) Sheikh Mohamed bin Zayed Al Nahyan, alipowatembelea wagonjwa wanaopatiwa matibabu katika hospitali moja mjini Abu Dhabi, walioumia kufuatia machafuko ya yanayoendelea Mashariki ya kati.

## Watanzania waliopo Dubai kurejeshwa

KONDOA

NA YUSUFU AMINI



# Dkt. Mwigulu: Kuhifadhi Qur'an kuendane na kuiishi kivitendo

Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Nchemba amewataka Waumini wa dini ya Kiislamu nchini kuhifadhi Kitabu Kitukufu cha Qur'an sambamba na kuyaishi mafundisho yake kivitendo. Pia amewasihi wadau na Waislamu kwa ujumla kuendelea kutumia majukwaa ya mashindano ya Qur'an kuhamasisha mapenzi ya Qur'an na si kushindana kuhifadhi Qur'an pekee.

Akizungumza wakati wa mashindano ya kusoma na kuhifadhi Qur'an wilaya ya Kondoa, Dkt. Mwigulu, ambaye alikuwa mgeni rasmi, alisema jamii ikifundishwa na kuelimishwa vizuri elimu ya dini, mambo mengi ambayo serikali inahangaika nayo hupungua au kuisha kabisa.

Aliongeza kuwa majukwaa yote ya mashindano ya Qur'an, walimu wa Qur'an, wazazi na walezi wanawajibika kuwafundisha kwa vitendo vijana wao kuhusu uchamungu, maadili mema, uadilifu, pamoja na kuhudumia na kuunganisha makundi mbalimbali katik jamii.

"Katika mashindano yetu haya ya leo, hakuna mshiriki ambaye amepoteza au ameshindwa, washiriki wote ni washindi kwa sababu mmejifunza, mmebeba Qur'an katika nyoyo zenu na mnaiendeleza Qur'an," alisema Dkt. Mwigulu na kuonya kuwa wazazi na walezi wasipowafundisha vijana kuwa wachamungu na watu wa ibada, ndivyo watakavyokuwa pindi watakapokuwa wakubwa.

Katika hotuba yake, Waziri Mkuu alieleza umuhimu wa kuendeleza maadili, elimu ya dini na mshikamano wa jamii kupitia mashindano ya kuhifadhi Qur'an tukufu. Ameeleza kuwa mashindano kama hayo yana mchango mkubwa katika kukuza malezi bora kwa vijana pamoja na kuimarisha misingi ya maadili mema katika jamii.

"Serikali inaunga mkono juhudi za taasisi za dini katika kuimarisha elimu ya kiroho na maadili kwa vijana. Malezi ya kidini yana nafasi muhimu katika kujenga jamii yenye amani, uvumilivu na mshikamano," alisema Dkt. Mwigulu.

Kuhusu umuhimu wa mashindano hayo, Waziri Mkuu alisema katika Qur'an sura ya pili aya ya 185, imeelezwa kuwa Qur'an imeshushwa ndani ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

"Mwezi wa Ramadhan ni mwezi wa kuisoma sana Qur'an kwa namna mbalimbali. Hongereni sana kwa kutekeleza agizo hili..., nilikuwa nawaangalia usoni watoto wetu hawa, nikawa naona siyo tu kwamba wanashindana mbele yetu, niliona ni kweli wamehifadhi Qur'an. Nilishangaa kuona tunaanza na juzuu tano, zikaja 10, halafu juzuu 20 na kisha juzuu 30," alisema.

Awali akimkaribisha Waziri Mkuu, Waziri wa Maliasili na Utalii ambaye pia ni Mbunge wa Kondoa vijijini, Dkt. Ashatu Kijaji, alisema mashindano hayo yamefanyika kwa miaka tisa mfululizo yakilenga kuandaa kizazi cha wachamungu.

"Wana Kondoa tunatamani kuona tunaandaa kizazi kilicho bora chenye kumjua Mungu. Kondoa tumeamua kuandaa Watanzania wenye hofu ya Mungu kwa kuwafundisha kitabu cha Mwenyezi Mungu, na niahidi kwamba ofisi ya Mbunge haitachoka kuandaa kazi hii," alisema Dkt. Kijaji.

Mashindano hayo yaliyofanyika kwenye uwanja wa Kambi ya Fisi, kijiji cha Bukulu wilayani Kondoa mkoa wa Dodoma yalihudhuriwa na viongozi mbalimali wa dini na serikali akiwamo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Mustafa Rajabu Shabani, Mwenyekiti wa CCM mkoa wa Dodoma, Adam Kimbisa, na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule.

## Zawadi kwa washindi

Washiriki wa kike na kiume kutoka maeneo mbalimbali wilayani Kondoa walishiriki katika ngazi tofauti za mashindano hayo kuanzia juzuu 1, 2, 3, 5, 10, 20 hadi 30.

Kwa washiriki wa juzuu 30, kijana Yassir Omary aliibuka mshindi wa kwanza na kuchukua kitita cha shilingi milioni moja, medali na mkoba maalum (paracel) wenye vifaa mbalimbali. Nafasi ya pili ilishikwa na Almasi Rashidi aliyepata shilingi laki nane, medali na paracel, na wa tatu ni Osama Ali aliyejinyakulia jumla ya shilingi laki sita, medali na paracel.

Kwa upande wa juzuu 20, mshindi wa kwanza ni Salim Yusuf aliyepewa laki tano, medali na paracel, mshindi wa pili ni Hamza Hamadi aliyepata laki nne, medali na paracel na wa tatu ni Anas Athumani aliyepewa laki mbili, medali na paracel.

NA MWANDISHI WETU



# Mwinyi ajumuika na maelfu futari ya kitaifa Zanzibar

**■ Asema Zanzibar imeandika historia ya kipekee kwa tukio hilo ■ Naibu Mufti wa Zanzibar, Sheikh Mahmoud Mussa Wadi, amesema Futari hiyo ya Kitaifa ni tukio muhimu linaloongeza mapenzi na upendo miongoni mwa Waumini, huku likichangia kuondoa chuki na kuimarisha mshikamano**

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwa Zanzibar imeandika historia ya kipekee kwa kuandaa Tukio Kubwa la Futari ya Kitaifa kwa mara ya kwanza, lililowakusanya maelfu ya Waumini wa Dini ya Kiislamu katika mkusanyiko wa pamoja.

Alhaj Dkt. Mwinyi ameyasema hayo alipotoa salamu zake kwa maelfu ya Waumini wa Dini ya Kiislamu waliohudhuria Futari hiyo ya Kitaifa iliyofanyika katika Uwanja wa New Amaan Complex, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Amesema tukio hilo ni jambo jema lenye thawabu kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu, sambamba na kuwa jukwaa muhimu la kuwaunganisha Waumini wa Dini ya Kiislamu pamoja na wananchi kwa ujumla katika kuimarisha mshikamano, upendo na umoja.

Aidha, Alhaj Dkt. Mwinyi amezishukuru taasisi za Serikali zilizoshirikiana kufanikisha Futari hiyo ya Kitaifa, ambazo ni Afisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar, Kamisheni ya Utalii Zanzibar pamoja na Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), kwa juhudi zao za kuandaa tukio hilo kubwa lililowakutanisha Waumini wengi katika mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Katika nasaha zake, Rais Dkt. Mwinyi amewataka Waumini kuendelea kuzidisha ibada, dua na matendo mema katika mwezi mtukufu wa Ramadhani, huku wakiendelea kumuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuijalia nchi amani, utulivu na mshikamano miongoni mwa wananchi wake.

Kwa upande wake, Naibu Mufti wa Zanzibar, Sheikh Mahmoud Mussa Wadi, amesema Futari hiyo ya Kitaifa ni tukio muhimu linaloongeza mapenzi na upendo miongoni mwa Waumini, huku likichangia kuondoa chuki na kuimarisha mshikamano kati ya makundi mbalimbali ya Waumini wa Dini ya Kiislamu.

رمضان

# MATUKIO KATIKA PICHA

Na Mpiga Picha Wetu



## Rais Dkt. Mwinyi ajumuika na maelfu futari ya kitaifa Zanzibar Uwanja wa New Amaan Complex









NA MWANDISHI WETU

# Mageuzi EAC yaamsha matumaini mapya ya ushirikiano

Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) imechukua maamuzi kadhaa makubwa yanayolenga kuimarisha uthabiti wa jumuiya hiyo baada ya miezi kadhaa ya changamoto za kifedha na wasiwasi unaoongezeka kuhusu kasi ya mchakato wa ushirikiano wa kikanda.

Katika Mkutano wa 25 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi wa EAC uliofanyika Arusha Jumamosi, viongozi walipitisha mfumo mpya wa uchangiaji wa kifedha, wakamteua Katibu Mkuu mpya na kumkabidhi Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, uenyekiti wa zamu wa jumuiya hiyo.

Maamuzi hayo yamefikiwa wakati jumuiya hiyo ya kikanda yenye wanachama wanane na zaidi ya watu milioni 300 ikiwa inakabiliwa na ucheleweshaji wa michango ya wanachama pamoja na maswali kuhusu ufanisi wa taasisi zake.

Moja ya maamuzi muhimu zaidi ni kupitishwa kwa mfumo mseto wa uchangiaji wa fedha.

Chini ya mfumo huo mpya, asilimia 50 ya bajeti ya EAC itachangiwa kwa usawa na nchi wanachama, huku asilimia 50 iliyosalia ikitokana na ukubwa wa uchumi wa kila nchi, unaopimwa kwa kutumia Pato la Taifa (GDP).

Mfumo huo mpya unachukua nafasi ya ule wa awali wa michango sawa kwa nchi zote, ambao ulikuwa ukikosolewa kwa kupuuza tofauti za kiuchumi kati ya nchi wanachama.

## Mwanateknokrasia aongoza Sekretarieti

Mkutano huo pia ulimteua mwanadiplomasia wa Tanzania, Stephen Mbundi, kuwa Katibu Mkuu mpya wa EAC kwa kipindi cha miaka mitano.

Awali wachunguzi walikuwa wakieleza kuwa jumuiya hiyo inahitaji kiongozi mwenye uwezo wa kitaalamu au mbunifu wa sera atakayesaidia kukabiliana na changamoto za taasisi zilizopo.

Bw Mbundi, ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ya Tanzania, analeta uzoefu wa karibu miongo mitatu katika diplomasia.

## Museveni achukua uenyekiti

Mabadiliko ya uongozi pia yalimshuhudia Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, akichukua rasmi uenyekiti wa zamu wa EAC. Mwenyekiti wa jumuiya hiyo ana jukumu muhimu la kisiasa katika kuelekeza mwelekeo wa kimkakati wa jumuiya na kuhakikisha viongozi wanatekeleza ahadi zilizotolewa chini ya Mkataba wa EAC.

## Wataalamu wanasema Museveni anakabiliwa na ajenda nzito.

"Mwenyekiti mpya anapaswa kurejesha imani katika mchakato wa ushirikiano wa kikanda kutokana na uzoefu wake katika uundaji wa jumuiya hiyo," alisema Dk Mvungi. "Ukanda huu una malengo makubwa, ikiwemo shirikisho la kisiasa, lakini maendeleo yamekuwa yasiyo sawa." Moja ya vipaumbele vya haraka itakuwa kuhakikisha nchi wanachama zinatekeleza makubaliano yaliyopo, hasa yale yanayohusu biashara, uhuru wa watu kusafiri na kuishi, pamoja na miundombinu ya kuunganisha nchi za kanda.

Licha ya changamoto zilizopo, wachambuzi wanasema mkutano wa Arusha umeweka angalau ramani ya njia ya kuimarisha uthabiti wa jumuiya hiyo ya kikanda.

Mchanganyiko wa mageuzi ya kifedha, uongozi mpya katika Sekretarieti na mamlaka mpya ya kisiasa kutoka kwa mwenyekiti unaweza kusaidia kuirejesha EAC katika mwelekeo wa maendeleo na kasi ya ushirikia-





Rais Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye mazungumzo na Rais wa Kenya kabla ya kuanza kwa mkutano wa wa wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya hiyo katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC). Picha na Ikulu

NA MWANDISHI WETU

# Rais Dkt. Mwinyi: Amani ni msingi wa maendeleo ya taifa

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amewasisitiza Waumini wa Dini ya Kiislamu pamoja na wananchi kuendelea kumuomba Mwenyezi Mungu kuijalia nchi amani zaidi.

Alhaj Dkt. Mwinyi ameyasema hayo, alipojumuika na Waumini wa Dini ya Kiislamu katika ibada ya Sala ya Ijumaa iliyosaliwa katika Msikiti wa Utheymin uliopo Mbweni kwa Jastuma, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Rais Dkt. Mwinyi amefahamisha kuwa majanga ya vita yanayoendelea katika nchi nyengine, akitolea mfano mzozo wa Mashariki ya Kati, yanatokana na kukosekana kwa maelewano na amani.

Ameeleza kuwa majanga hayo yamekuwa yakiathiri nchi mbalimbali duniani kiuchumi na kijamii. Alhaj Dkt. Mwinyi amesema ni vema kwa waumini kuendelea kuiombea amani nchi Zanzibar kwani bila ya amani hakuna jambo lolote la maendeleo linaloweza kufanyika.

Wakati huo huo, Rais Dkt. Mwinyi amewanasihi Waumini wa Dini ya Kiislamu kuongeza juhudi katika kutekeleza ibada wakati huu wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ukiwa katika kumi la pili.



HABARI MOROGORO

NA MWANDISHI WETU

# Mtandao wa utapeli wanaswa Morogoro



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Alex Mkama

**Jeshi la Polisi mkoani Morogoro limekamata laini za simu 198 zinazotumika kwa utapeli. Kati ya laini hizo, 88 zimekamatwa kwa wakala wa kusajili laini za simu na zimesajiliwa kwa majina tofauti.**

Wakati ripoti ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ya Desemba mwaka jana ikiutaja Mkoa wa Morogoro kuwa wa pili kwa matukio ya ulaghai kupitia simu za mkononi, Jeshi la Polisi mkoani humo limekamata laini za simu 198 zinazotumika kwa utapeli.

Kati ya laini hizo, 88 zimekamatwa kwa wakala wa kusajili laini za simu na zimesajiliwa kwa majina tofauti.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Alex Mkama, aliwaambia waandishi jana kuwa wamekamata watuhumiwa 10 wanaodaiwa kufanikiwa kuwaibia baadhi ya waathirika zaidi ya Sh12 milioni katika eneo la Mbagala, mkoani Dar es Salaam, kwa kutumia mbinu za ulaghai kupitia simu.

Hayo yanafanyika wakati TCRA ilishatangaza kumaliza tatizo la utapeli wa simu kwa kila laini kusajiliwa kwa alama za vidole, hasa kwa matapeli wa 'tuma kwenye namba hii.'

Alipoulizwa kuhusu kuendelea kuwepo kwa mbinu za utapeli na udhibiti wake ulipofikia, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma TCRA, Rolf Kibaja, alisema taasisi hiyo inahusika na masuala ya usalama pekee na hawashughuliki na masuala ya uhalifu na utapeli.

Alisema kazi hiyo imekuwa ikifanywa na wale wanaokwenda kukamata watuhumiwa husika.

Kibaja alisema kazi kubwa ya TCRA ni kutoa elimu kwa umma, na wanahakikisha wananchi wanajua mambo muhimu wanayopaswa kufanya kwenye mtandao.

"Tumeweka namba 15040. Kukiwa na suala lolote la utapeli au mtu anataka kukutumia taarifa yenye uhalifu, unatuma hiyo kwenye namba hiyo. Tunawaambia wananchi wahakiki laini zao za simu kwa kupiga *106#," alisema na kuongeza:



"Tunahamasisha watu wasipokee maelekezo yoyote kutoka kwa watu isipokuwa kupitia namba 100 ya mtoa huduma. Namba tofauti na 100 si ya mtoa huduma."

Kibaja alisema kazi ya kuendelea kutoa elimu kwa umma ni ngumu, kwani wanaweza kutoa elimu lakini mwananchi asipochukua hatua anaweza kujikuta ameingia kwenye hatua mbaya.

Hata hivyo, Kamanda Mkama aliwaambia waandishi wa habari kuwa katika operesheni maalumu walikamata watuhumiwa 10 wa utapeli.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa Machi 3, mwaka huu, katika operesheni maalumu iliyofanyika Kitongoji cha Magoha, Kata ya Lumemo, Mji wa Ifakara, wilayani Kilombero.

Mkama alisema kuwa katika operesheni hiyo watuhumiwa saba walikamatwa wakiwa na laini 110 za simu za mitandao mbalimbali.

NA MUGINI SINGIRA



# Mufti akemea wanaotumia dini kuvuruga amani

Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeir bin Ally ametoa rai kwa Waumini wa dini ya Kiislamu nchini, viongozi mbalimbali pamoja na Watanzania kwa ujumla kuwapuuza watu wanaoeneza chuki za kidini, akisisitiza umuhimu wa kuendelea kuishi kwa upendo, umoja na kuvumiliana kama alivyofundisha Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani imshukie).

Mufti alitoa kauli hiyo Machi 4, 2026 wakati akisoma tamko la maazimio ya kikao cha Baraza la Ulamaa kilichofanyika makao makuu ya Bakwata, Kinondoni jijini Dar es Salaam. Katika tamko hilo, Mufti Zubeir aliwasihi Waislamu kutokubali kuchokozeka na watu wachache wanaoeneza ujumbe wa kumtukana Mtume, kuukashifu Uislamu na kuibeza dini hiyo.

"Tunaamini wanaofanya hayo si Wakristo wala watu wa dini nyingine yeyote, bali ni watu wenye nia ovu ya kutuchonganisha ili tugombane na kusababisha mtafaruku kati yetu na dini nyingine pamoja na jamii kwa ujumla. Niwasihi Waislamu wasiingie kujibizana kwa sababu watu hao wanataka kueneza chuki na fitna dhidi ya dini nyingine," alisema Mufti Zubeir.

Aidha, Mufti amewataka Waislamu wote nchini wakiwamo Masheikh, wanazuoni, maimamu, walimu wa dini pamoja na jamii kwa ujumla kuendelea kuishi kwa upendo, kuvumiliana na kudumisha umoja wa kitaifa uliodumu kwa muda mrefu nchini.

"Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) aliishi na wasiokuwa Waislamu kwa wema na alishirikiana nao kwa amani," amesisitiza.

Katika hatua nyingine, Mufti Zubeir amewataka Waislamu na Watanzania kwa ujumla kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa mbalimbali ikiwamo Covid–19, Hepatitis, Dengue Fever na kipindupindu kwa kufuata maelekezo yanayotolewa na serikali. Pia amewatakia Waislamu wote mfungo mwema wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Afya
Pure Drinking water
"Afya"is natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.
WATERCOM LIMITED
P.o. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email:info@watercomtz.com


UKHTI FATUMA SS

# Rais UAE aionya Iran: Falme za Kiarabu si mawindo rahisi

Rais wa Falme za Kiarabu (UAE), Mohamed bin Zayed Al Nahyan, amejitokeza hadharani kuwafariji watu waliojeruhiwa katika mashambulizi ya Iran na kuahidi kulinda taifa hilo, akisisitiza kuwa UAE haitakuwa "mawindo rahisi" katika mgogoro unaoendelea Mashariki ya Kati.

Kiongozi huyo alitoa kauli hiyo alipowatembelea majeruhi katika hospitali moja nchini humo, akionyesha mshikamano na raia na wakazi wa kigeni wanaoishi katika taifa hilo wakati wa hali ya mvutano wa kijeshi.

"UAE ina ngozi ngumu na nyama chungu – sisi si mawindo rahisi," alisema katika kauli iliyotangazwa na vyombo vya habari vya serikali, akiahidi kuwa serikali itatimiza wajibu wake wa kulinda nchi, wananchi na wakazi wote wanaoishi humo.

Kwa mujibu wa ripoti za Al Jazeera na Reuters, Rais bin Zayed aliwatembelea majeruhi watano waliumia katika mashambulizi hayo, wakiwemo raia wawili wa UAE pamoja na watu kutoka India, Sudan na Iran. Alisema majeruhi hao ni "jukumu lililo mabegani mwetu" na serikali itaendelea kuwahudumia.

Katika hotuba yake, kiongozi huyo pia aliwashukuru wanajeshi na vyombo vya usalama vya UAE kwa jukumu lao katika kulinda nchi wakati wa mgogoro huo.

Mashambulizi hayo yanatokea katika muktadha wa mvutano mkubwa unaoendelea katika eneo la Mashariki ya Kati. Tangu Februari 28, Marekani na Israel zimekuwa zikishambulia malengo nchini Iran, huku Tehran ikijibu kwa kurusha makombora na ndege zisizo na rubani katika maeneo kadhaa ya kanda hiyo.

Baadhi ya mashambulizi hayo yameripotiwa kugonga miundombinu na maeneo ya kiraia katika nchi kadhaa za Ghuba.

Hata hivyo, Rais bin Zayed alisema licha ya hali hiyo, UAE itaendelea kulinda kila mtu ndani ya mipaka yake na ina imani kuwa taifa hilo litatoka katika kipindi hicho cha mgogoro likiwa na nguvu zaidi.



Rais wa Falme za Kiarabu (UAE) Sheikh Mohamed bin Zayed Al Nahyan, alipowatembelea wagonjwa wanaopatiwa matibabu katika hospitali moja mjini Abu Dhabi, walioumia kufuatia machafuko ya yanayoendelea Mashariki ya kati.

NA MUGINI SINGIRA

# Watanzania waliopo Dubai kurejeshwa

Serikali imeanza kuchukua hatua za haraka na za kiutendaji ili kuhakikisha Watanzania waliopo jiji la Dubai katika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) wanarejeshwa salama nchini.

Uamuzi huo umetokana na mgogoro unaoendelea kushamiri baina ya mataifa ya Israel na Marekani dhidi ya Iran, hali ambayo imesababisha baadhi ya nchi kuanza kuchukua hatua za dharura za kuwarejesha raia wao waliopo kwenye maeneo yanayoathiriwa na mgogoro huo.


Taarifa ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) iliyotolewa Machi 6, 2026 imeeleza kuwa, safari hiyo maalum itafanyika siku ya Jumapili Machi 8, 2026 kwa abiria wenye tiketi walioathirika na kusitishwa kwa safari za ndege Mashariki ya Kati. Vilevile, safari hiyo pia itawahusu abiria waliokwama nchini ambapo watasafirishwa hadi Dubai.

Taarifa hiyo imekuja ikiwa zimepita siku sita tangu ATCL itangaze kusitisha safari zake kuelekea Dubai baada ya kufungwa kwa anga la Mashariki ya Kati kulikosababishwa na vita hiyo iliyoanza Februari 28, 2026

"Safari hii ya ndege imeandaliwa mahsusi kwa ajili ya kuwarejesha abiria majumbani mwao na siyo safari ya kawaida ya kibiashara. Kipaumbele kitatolewa kwa abiria waliokuwa na tiketi halali za safari ya Dar es Salaam kwenda Dubai ambayo awali iliathirika," imesema sehemu ya taarifa hiyo.

Katika hatua nyingine, ATCL imewashauri abiria kuwasiliana na ofisi za shirika hilo kwa maelekezo na uthibitisho wa usafiri kabla ya kuondoka, ikiwataka kutumia namba +255 748 773 900 kwa waliopo Dar es Salaam na namba +971 54 464 5322 kwa waliopo Dubai.

Awali, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilisema inaendelea kufuatilia kwa karibu hali ya usalama inayoendelea Mashariki ya Kati huku ikiwataka wananchi waliopo eneo hilo kuchukua hatua stahiki kulinda usalama wao.



Baadhi ya abiria wa kigeni waliokwama kusafiri kutoka Dubai kutokana na mzozo wa vita vinavyoendelea Mashariki ya kati

UKHTI FATIMA SS

# Namna Tanzania inaweza itaathirika kiuchumi kwa vita ya Mashariki ya Kati

Vita vinavyoendelea Mashariki ya Kati vinaonekana kuwa mbali kijiografia na Tanzania, lakini wachambuzi wa uchumi wanaonya kuwa athari zake zinaweza kufika haraka kupitia bei za mafuta, chakula na biashara ya kimataifa.

Uchumi wa Tanzania, kama ilivyo kwa nchi nyingi za Afrika, umeunganishwa na mifumo ya kimataifa ya biashara na nishati, hivyo misukosuko katika eneo hilo inaweza kuathiri maisha ya kila siku ya wananchi.

Athari ya kwanza inayotajwa zaidi na wataalamu ni kupanda kwa bei ya mafuta. Mashariki ya Kati ni chanzo kikubwa cha mafuta duniani, na sehemu muhimu ya usafirishaji wake hupitia Mlango wa Bahari wa Hormuz. Kwa mujibu wa uchambuzi ulioripotiwa na CNN na BBC, njia hiyo hubeba takribani asilimia 20 ya mafuta ya dunia.

Endapo usafirishaji utavurugika, bei ya mafuta duniani hupanda haraka. Kwa nchi kama Tanzania inayotegemea kuagiza mafuta kutoka nje, hali hiyo inaweza kuongeza gharama za usafiri, umeme na uzalishaji wa viwandani.

Athari ya pili ni ongezeko la bei ya chakula. Ripoti ya CNN inaeleza kuwa vita vinaweza kuathiri pia usafirishaji wa mbolea na malighafi za kilimo. Takribani theluthi moja ya mbolea ya urea duniani hupitia njia za usafiri wa Mashariki ya Kati. Tayari bei ya mbolea imeanza kupanda katika masoko ya kimataifa.

Kwa Tanzania na Afrika kwa ujumla—ambako kilimo kinategemea sana mbolea za kuagiza—ongezeko hilo linaweza kuongeza gharama za uzalishaji na hatimaye kupandisha bei ya chakula.

Athari nyingine ni usumbufu katika biashara na usafirishaji wa bidhaa. Vita vinaweza kufanya baadhi ya njia za baharini kuwa hatari au ghali kutokana na gharama za bima na ulinzi wa meli. BBC inaeleza kuwa gharama za usafirishaji wa mafuta kwa meli kubwa zimeongezeka mara mbili ndani ya siku chache kutokana na hatari za usalama. Gharama hizi zikiongezeka, bidhaa nyingi zinazoingia Afrika—kutoka vifaa vya viwandani hadi bidhaa za matumizi—zinaweza kuwa ghali zaidi.

Kwa mtazamo mpana zaidi, wachumi wanaonya kuwa vita vinaweza pia kuongeza mfumuko wa bei duniani. Uchambuzi wa wachumi ulioripotiwa na The Guardian la Uingereza unaonyesha kuwa kupanda kwa bei ya nishati kunaweza kusababisha benki kuu duniani kupandisha kuchukua hatua za kudhibiti mfumuko wa bei. Hali hiyo inaweza kupunguza uwekezaji na biashara katika nchi zinazoendelea.

Kwa hiyo, ingawa vita vinaendelea maelfu ya kilomita mbali, uchumi wa Tanzania unaweza kuyahisi maumivu kupitia bei katika soko la ndani na mwenendo wa biashara ya kimataifa.



NA MWANDISHI WETU

# Vita Iran, Marekani vyachochea makali bei ya mafuta

Vita kati ya Marekani na Israel dhidi ya Iran vinaweza kusababisha bei za mafuta kupanda kwa muda mrefu zaidi duniani, hata kama mzozo huo uliodumu kwa wiki moja utamalizika haraka, kutokana na uharibifu wa miundombinu, kuvurugika kwa usafirishaji na hatari kubwa kwa meli zinazobeba mafuta.

Matarajio hayo yanaweka shinikizo kwa uchumi wa dunia na pia yanaweza kuwa changamoto ya kisiasa kwa Rais wa Marekani, Donald Trump hasa kuelekea uchaguzi wa katikati ya muhula, wakati wapigakura huwa makini kwenye gharama za nishati na mara nyingi hupinga kuhusika kwa nchi yao katika migogoro ya nje.

Kwa mujibu wa Reuters, wachambuzi wa Benki ya Uwekezaji JPMorgan Chase walisema katika ripoti ya utafiti Ijumaa iliyopita kuwa, soko la mafuta sasa linaanza kukabiliana si tu na hatari za kisiasa bali pia na athari halisi za kiutendaji.

“Soko linaondoka kwenye kukadiria hatari za kisiasa pekee na sasa linakabiliwa na usumbufu wa moja kwa moja wa shughuli huku kufungwa kwa baadhi ya mitambo ya kusafisha mafuta na vikwazo vya usafirishaji vikianza kuathiri uchakataji wa mafuta ghafi na mtiririko wa usambazaji wa kikanda,” walieleza wachambuzi.

Mzozo huo tayari umeathiri takribani asilimia 20 ya usambazaji wa mafuta ghafi na gesi asilia duniani, baada ya Iran kulenga meli katika Mlango Bahari wa Hormuz, njia muhimu ya usafirishaji wa nishati kati ya pwani zake na Oman, pamoja na kushambulia miundombinu ya nishati katika eneo hilo.

Bei za mafuta duniani tayari zimepanda kwa zaidi ya asilimia 25 tangu vita hivyo kuanza, hali inayosababisha gharama za mafuta kupanda kwa watumiaji duniani.

Kufungwa karibu kabisa kwa Mlango Bahari wa Hormuz kumelazimisha wazalishaji wakubwa wa mafuta wa Saudi Arabia, Falme za Kiarabu (UAE), Iraq na Kuwait kusitisha usafirishaji wa hadi mapipa milioni 140 ya mafuta, sawa na mahitaji ya dunia kwa takribani siku 1.4.

Kutokana na hali hiyo, hifadhi za mafuta na gesi katika vituo vya Ghuba ya Mashariki ya Kati zinaanza kujaa haraka na kulazimisha baadhi ya visima vya mafuta nchini Iraq na Kuwait kupunguza uzalishaji. Wachambuzi wamesema huenda UAE nayo ikafuata hatua hiyo.

“Muda si mrefu kila mtu atalazimika kusimamisha uzalishaji ikiwa meli hazitafika kuchukua mafuta,” kilieleza chanzo kimoja kutoka kampuni ya mafuta inayomilikiwa na Serikali katika eneo hilo, kama kilivyonukuliwa na Reuters.




Kwa mujibu wa Amir Zaman wa kampuni ya utafiti wa nishati ya Rystad Energy, visima vya mafuta vitakavyolazimika kufungwa katika Mashariki ya Kati kutokana na kuvurugika kwa usafirishaji vinaweza kuchukua muda kurejea katika uzalishaji wa kawaida.

Ikulu ya Marekani ilihalalisha mashambulizi dhidi ya Iran kwa kusema nchi hiyo ilikuwa tishio la haraka kwa Marekani, ingawa haijatoa maelezo ya kina. Rais Trump pia amesema ana wasiwasi kuhusu juhudi za Iran kutafuta silaha za nyuklia.

## Hatari iliyopo Hormuz

Kumalizika kwa haraka kwa vita kunaweza kutuliza masoko ya nishati, lakini kurejea kwa usambazaji na bei katika viwango vya kabla ya vita kunaweza kuchukua wiki au hata miezi, kutegemea na kiwango cha uharibifu wa miundombinu na usafirishaji.

“Kwa sasa hatujaona uharibifu mkubwa wa kudumu katika miundombinu kutokana na mashambulizi ya Iran, ingawa hatari bado ipo kadiri vita vinavyoendelea,” alisema Joel Hancock, mchambuzi wa nishati wa Natixis Corporate & Investment Banking.

Swali kubwa kwa sasa ni lini na kwa kiwango gani mlango Bahari wa Hormuz utakuwa salama tena kwa usafirishaji wa meli za mafuta. Trump aliahidi kutoa ulinzi wa kijeshi kwa meli za mafuta pamoja na msaada wa bima ya Marekani kwa meli zinazopita katika eneo hilo.

UKHTI FATIMA SS

# Kwa nini Urusi na China wamemwacha Iran?

Kadiri mashambulizi dhidi ya Iran yanavyozidi, swali moja limekuwa kubwa: wako wapi washirika wake wakubwa, Urusi na China? Jibu fupi ni hili: wanaisemea Iran kidiplomasia, lakini hawako tayari kuipigania kijeshi. Hilo linaonyesha kwamba si kila ushirikiano wa kisiasa ni muungano wa vita.

Kwa upande wa Urusi, sababu ya kwanza ni ya kisheria na kimkakati. Al Jazeera inaeleza kuwa makubaliano ya ushirikiano kati ya Moscow na Tehran yaliyosainiwa Januari 2025 hayakuwa mkataba wa ulinzi wa pamoja. Hivyo, Urusi haina wajibu wa kuingia vitani kwa niaba ya Iran kama ilivyo katika baadhi ya miungano rasmi ya kijeshi.

Sababu ya pili ni kwamba Urusi ina vita vyake tayari: Ukraine. Reuters ilinukuu wachambuzi wakisema Kremlin haitaki kufungua uwanja mwingine wa mgogoro wa moja kwa moja na Marekani wakati bado imezama Ukraine. Kwa lugha rahisi, Putin anaona gharama ya kuitetea Iran kuwa kubwa kuliko faida yake. Zaidi ya hapo, Urusi haitaki kuharibu uhusiano wake na nchi za Ghuba na Israel, ambazo zote zina uzito wa kisiasa na kiuchumi katika eneo hilo.

Lakini pia kuna hesabu ya faida. Reuters inaonyesha kuwa kupanda kwa bei ya mafuta kutokana na vita kunaweza kuisaidia Urusi, kwa sababu mapato yake ya nishati yanaongezeka. Aidha, Marekani ikijikita zaidi Mashariki ya Kati, shinikizo kwa Urusi katika vita vya Ukraine linaweza kupungua. Kwa hiyo, Moscow inaweza kuona mgogoro huu kama tatizo kwa Iran, lakini si lazima kama hasara kwa Urusi.

China nayo ina mantiki tofauti, lakini hitimisho ni lilelile: haitaki vita. Al Jazeera inaeleza kuwa Beijing imejenga uhusiano mkubwa wa kiuchumi na Iran, hasa katika nishati, lakini imeweka mipaka wazi kuhusu msaada wa kijeshi. Mtazamo wake wa muda mrefu ni kutokuingia moja kwa moja katika migogoro ya kijeshi ya mbali na maslahi yake ya msingi.

Reuters inaongeza kuwa China ina uhusiano mpana zaidi kuliko Iran pekee; ina biashara, uwekezaji na maslahi ya nishati pia kwa nchi za Ghuba. Hivyo, haiwezi "kuweka mayai yake yote kwenye kikapu cha Iran." Badala ya kupigana, Beijing inapendelea kujiweka kama mpatanishi, huku ikilinda biashara na usalama wa nishati yake.

Hitimisho ni wazi: Iran ni mshirika muhimu kwa Urusi na China, lakini si muhimu kiasi cha wao kuhatarisha vita vya moja kwa moja na Marekani kwa ajili yake. Huu ni ukumbusho mkali wa siasa za kimataifa: mataifa hayana marafiki wa kudumu, yana maslahi ya kudumu.





HABARI MASHARIKI YA KATI

MAHMOUD NYAMGUMA

# Israel yazuia sala ya Ijumaa Al-Aqsa

Mamlaka za Israel zimefunga maeneo yote matakatifu katika Mji wa Kale wa Jerusalem Mashariki, ikiwemo Msikiti wa Al-Aqsa.

Hatua hiyo inayohusishwa na hali tete ya usalama kutokana na vita ya taifa hilo la kizayuni dhidi ya Iran na kundi la Hizbullah la Lebanon, imekuja wakati Waislamu wakiwa katikati ya mwezi mtukufu wa Ramadhan.


Malalamiko makubwa yameibuka kutoka kwa Waislamu wanaoona kuwa huo ni mwendelezo wa sera za kudhibiti ibada katika msikiti huo wa tatu kwa utukufu duniani, likitanguliwa na misikiti mikuu ya Makka (Masjid al-Haram) na Madina (Masjid Nnabawi).

Kwa kawaida, kila Ijumaa ya Ramadhan, Waumini 50,000 hadi 100,000 hukusanyika Al-Aqsa kusali, kulingana na takwimu za Waqf ya Kiislamu ya Al- Quds.

Mji wa Kale wa Al-Aqsa uko katika eneo la Jerusalem Mashariki ambalo Israel ililiteka mwaka 1967 wakati wa Vita vya Siku Sita na kutangaza kulimiliki, hatua isiyotambuliwa na jumuiya kubwa ya kimataifa ikiwemo Umoja wa Mataifa.

Hatua kali za vikwazo kwa Wapalestina kuingia eneo la Al-Aqsa vimeongezeka maradufu tangu Oktoba 2023, Israel ilipoanza kampeni mpya ya ukandamizaji dhidi ya Israel.

Al-Aqsa ni msikiti wa tatu kwa utukufu katika Uislamu, hivyo hatua yoyote inayozuia ibada katika eneo hilo mara nyingi huchukuliwa kama suala la kisiasa, kidini na haki za msingi za Waumini wa Kiislamu.



## HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU




# Rais Museveni azindua kampuni ya kwanza ya bima ya Kiislamu Uganda

Rais wa Uganda, Yoweri Kaguta Museveni, amezindua kampuni ya kwanza ya bima ya Kiislamu nchini humo huku akisifu takaful kwa kuendana na utamaduni wa asili wa Kiafrika wa kusaidiana kijamii.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Tamini General Insurance jijini Kampala, Museveni alisema mfumo huo wa bima unafanana na misingi ya kijamii iliyokuwepo barani Afrika kwa muda mrefu.

"Hili si jambo geni; ni utamaduni wetu wa zamani wa kusaidiana — omukwato," Museveni alinukuliwa akisema wakati wa hafla ya Iftar iliyofanyika Lugogo.

Kampuni hiyo mpya ya bima ya Kiislamu, Tamini General Insurance, ni sehemu ya Salaam Group na inafanya kazi kwa ushirikiano na Salaam Bank Uganda, benki ya kwanza ya Kiislamu nchini Uganda iliyozinduliwa mwaka 2024.

Kwa mujibu wa taarifa zilizochapishwa na vyombo vya habari ikiwemo Garowe Online na PML Daily, kuanzishwa kwa kampuni hiyo kunapanua mfumo wa huduma za kifedha zinazofuata misingi ya Sharia nchini Uganda, baada ya marekebisho ya sheria ya taasisi za fedha mwaka 2023 kuruhusu rasmi benki na huduma nyingine za kifedha za Kiislamu.

Bima ya Kiislamu, inayojulikana kama Takaful, inafuata kanuni za kusaidiana na kugawana hatari, tofauti na bima ya kawaida ambayo hatari inahamishwa kwa kampuni. Aidha, washiriki wa Takaful huchangia katika mfuko wa pamoja unaotumika kufidia wanachama wanapopata hasara.




Mwenyekiti wa Salaam Bank Uganda, Ibrahim M. Abdirahman, alisema huduma hizo zinalenga kuwafikia wananchi ambao kwa muda mrefu walikuwa wakiepuka mfumo wa kawaida wa fedha kutokana na sababu za kidini au kimaadili.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa Tamini Insurance Group, Mohamed Bahdon, alisema bima hiyo itasaidia kulinda uwekezaji wa wananchi na biashara kupitia mfumo wa kifedha unaozingatia maadili na uwazi.

Kwa mujibu wa PML Daily, kiwango cha watu wenye bima nchini Uganda bado ni kidogo sana, kikiwa chini ya asilimia moja ya wananchi. Hali hiyo inaonyesha fursa kubwa ya ukuaji wa sekta ya bima ya Kiislamu katika nchi hiyo.

Maafisa wa udhibiti wa bima wanaamini kuwa kuanzishwa kwa Takaful kutapanua upatikanaji wa bima, kuongeza ujumuishaji wa kifedha na kusaidia kukuza uchumi kwa kuwapa wananchi njia mbadala ya kulinda mali na uwekezaji wao.

# Indonesia kuharakisha ukuaji sekta halal kwa kuimarisha uthibitishaji bidhaa

**Serikali ya Indonesia imeweka mkakati wa kuharakisha ukuaji wa sekta ya bidhaa na huduma za halal mwaka 2026, ikilenga kuimarisha mfumo wa uthibitishaji wa bidhaa na kuongeza utambuzi wa kimataifa wa vyeti vya halal vya nchi hiyo.**

**Kwa mujibu wa shirika la habari la Indonesia Antara News, Mkuu wa Wakala wa Uhakiki wa Bidhaa Halal (BPJPH], Ahmad Haikal Hasan, alisema mwaka 2026 ni fursa muhimu ya kuimarisha mfumo wa sekta ya halal nchini humo na kuongeza mchango wake katika uchumi wa taifa.**

**Hasan alisema kuwa mwaka 2025, mfumo wa thamani wa sekta ya halal ulichangia takribani asilimia 27 ya pato la taifa (GDP] la Indonesia, sawa na rupia trilioni 4,832 au karibu dola za Marekani bilioni 81.5. Takwimu hizo zinaonyesha kuwa sekta hiyo imekuwa mhimili muhimu wa uchumi katika taifa hilo lenye idadi kubwa ya Waislamu duniani.**

**Ili kuimarisha ukuaji huo, BPJPH inapanga kupanua ushirikiano wa kimataifa katika utambuzi wa vyeti vya halal. Tayari taasisi hiyo imesaini makubaliano ya kutambuana vyeti vya halal na taasisi kutoka China, Ufilipino na Mexico.**

**Serikali pia inalenga kuunganisha maendeleo ya sekta ya halal na mifumo ya fedha za Kiislamu kama vile zakat na waqf ili kuongeza ujumuishaji wa kiuchumi.**

**Indonesia tayari inashika nafasi ya tatu duniani katika uchumi wa Kiislamu, na serikali yake inalenga kuifanya nchi hiyo kuwa kitovu cha kimataifa cha uchumi wa Kiislamu katika miaka ijayo.**




# Jukwaa uwekezaji wa halal lafungua fursa kwa Wamarekani




Wawekezaji wa Kiislamu nchini Marekani wameanza kupata fursa mpya ya kuwekeza katika masoko ya mitaji kwa njia inayozingatia misingi ya Sharia, kufuatia kuanzishwa kwa jukwaa maalumu la uwekezaji wa halal.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa na Crowdfund Insider, jukwaa hilo jipya linawalenga hasa wawekezaji wanaotaka kushiriki katika soko la hisa la Marekani bila kuingia katika shughuli zinazokinzana na kanuni za Kiislamu kama riba, kamari au uwekezaji katika sekta zinazokatazwa.

Taarifa hiyo inaeleza kuwa kwa muda mrefu wawekezaji wa Kiislamu wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya kupata zana zinazoweza kuwasaidia kuchuja uwekezaji unaokubalika kidini. Mara nyingi walilazimika kutumia mifumo tofauti kwa ajili ya kuchunguza uhalali wa hisa, kufanya biashara na kufuatilia uwekezaji wao.

Jukwaa hilo linakusudia kurahisisha mchakato huo kwa kuweka pamoja huduma za kuchuja uwekezaji, kufanya biashara ya hisa na kusimamia uwekezaji katika mfumo mmoja. Mfumo huo pia husaidia wawekezaji kufuatilia mapato yasiyoruhusiwa na kufanya marekebisho ya kisheria kama vile utakaso wa mapato na hesabu za zakat.

Wataalamu wa sekta ya fedha wanaeleza kuwa mahitaji ya uwekezaji unaozingatia maadili ya Kiislamu yanaendelea kukua kwa kasi duniani. Makadirio yanaonyesha kuwa thamani ya sekta ya fedha za Kiislamu inaweza kufikia dola trilioni 9.7 ifikapo mwaka 2029.

Hata hivyo, majukwaa ya kidijitali bado yanachangia sehemu ndogo tu ya soko hilo, jambo linaloonyesha nafasi kubwa ya ukuaji kwa mifumo ya teknolojia ya kifedha inayolenga wawekezaji wanaotafuta uwekezaji unaoendana na misingi ya kimaadili na kidini.

## Vita Mashariki ya Kati yasababisha taharuki ya usafiri

**Zaidi ya safari 14,000 za ndege zimefutwa Mashariki ya Kati tangu kuanza kwa mashambulizi dhidi ya Iran, hali iliyosababisha mamia ya maelfu ya wasafiri kukwama katika viwanja vya ndege huku sekta ya usafiri wa anga ikikumbwa na usumbufu mkubwa.**

**Kwa mujibu wa CNN, takwimu za mfumo wa kufuatilia safari za ndege wa Flightradar24 zinaonyesha kuwa kufutwa kwa safari hizo kulianza Februari 28, baada ya mashambulizi ya Marekani na Israel dhidi ya Iran.**

**Angalau nchi 10 katika eneo hilo zililazimika kufunga anga zao kabisa au kwa sehemu kutokana na hali ya usalama.**

**Anga za Mashariki ya Kati, ambazo kwa kawaida huwa na shughuli nyingi za ndege, zimeonekana kupungua kwa kiasi kikubwa cha safari. Uwanja wa ndege wa Dubai International—moja ya vituo vikubwa vya usafiri wa anga duniani—ulipunguza safari zake kwa asilimia 85 tangu mashambulizi hayo kuanza. Sharjah ilifuta karibu asilimia 90 ya safari zake, huku Doha nchini Qatar ikifuta takribani asilimia 94 ya safari zilizopangwa.**

**Miongoni mwa walioathirika zaidi na usumbufu huo ni mahujaji wa Umrah waliokuwa wakirejea nyumbani kutoka Saudi Arabia. Ripoti ya Khaleej Times inaeleza kuwa baadhi ya mahujaji waliokuwa wakirejea Falme za Kiarabu walilazimika kusafiri kwa basi kutoka Madina hadi Dammam kisha kuelekea mpaka wa Al Batha ili kupata usafiri wa kuingia UAE baada ya safari zao za ndege kusitishwa.**

**Wakati huo huo, karibu mahujaji 2,000 kutoka Jammu na Kashmir nchini India wameripotiwa kukwama katika miji ya Makka, Madina na Jeddah wakisubiri ratiba mpya za ndege, kulingana na taarifa ya The Kashmir Images.**

**Licha ya hali hiyo, baadhi ya viwanja vya ndege vimeanza kurejesha shughuli taratibu, ikiwemo Dubai, Abu Dhabi na King Khalid International karibu na Riyadh, ingawa hali ya safari za anga bado inaendelea kutegemea mwenendo wa mgogoro katika eneo hilo.**

## Matawi ya benki za Kiislamu Pakistan yafikia 40% ya mtandao wa benki

**Pakistan inaendelea kushuhudia ongezeko kubwa la huduma za benki zinazofuata misingi ya Kiislamu, huku zaidi ya asilimia 40 ya matawi ya benki nchini humo sasa yakitoa huduma za benki za Kiislamu.**

**Takwimu hizi zinaonyesha mabadiliko makubwa katika mfumo wa fedha wa nchi hiyo kuelekea huduma zisizohusisha riba.**

**Kwa mujibu wa ripoti iliyochapishwa na Pro-Pakistani, Benki Kuu ya Pakistan (State Bank of Pakistan] imeeleza kuwa hadi mwisho wa mwaka 2025 kulikuwa na matawi 7,562 ya benki za Kiislamu pamoja na "windows" 2,931 zinazotoa huduma hizo ndani ya benki za kawaida. Matawi hayo yanaendeshwa na benki kamili za Kiislamu pamoja na vitengo vya benki za Kiislamu vilivyopo katika benki za kawaida.**

**Takwimu hizo zinaonyesha ongezeko kubwa ikilinganishwa na mwaka uliotangulia, ambapo benki za Kiislamu zilikuwa zikichangia asilimia**

رمضان

MAKALA MAALUM

0783 650 803

SAID RAJAB



# Umuhimu wa tafakuri katika Uislamu

Allah 'Azza Wajallah' amewapa wanadamu uwezo wa kufikiri na kutafakari. Ni uwezo huu unaowafanya wanadamu wawe tofauti na wanyama, na kuwafanya wawe na utashi huru ikilinganishwa na viumbe wengine wote.

Kwa neema hii, ambayo Allah 'Azza Wajallah' ametujaalia, tunaweza kuishi na kustawi katika ulimwengu huu. Bila ya neema hii ya Mwenyezi Mungu, hatuwezi kuendelea katika ulimwengu huu na wala hatutaweza kupata wokovu kesho Akhera.

Kwa hiyo tunaona kwamba, kufikiri, kutafakari na kuakisi mambo ndiyo ufunguo muhimu unaotuongoza kwa Mwenyezi Mungu, ambaye mara kwa mara anatuelekeza ndani ya Qur'an Tukufu kuakisi na kuutafakari ulimwengu huu (universe).

Ndani ya surat Al–Imran kuna aya zinasema: "Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na kuhitilafiana usiku na mchana, bila shaka ziko Ishara (dalili, mazingatio) kwa wenye akili. Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima, au wamekaa, au wamelala, na wanatafakari katika kuumbwa mbingu na ardhi, wakisema: Mola wetu Mlezi! Hukuumba haya bure. Umetakasika! Basi tukinge na adhabu ya Moto." [Qur'an, 3:190–191].

Kutoka kwenye aya hii, tunaweza kuona kwamba watu wenye uelewa na tafakuri kuhusu ulimwengu, Allah huwaongoza katika kugundua uhalisia wa kuwepo kwa Mwenyezi Mungu. Wanapoona mpangilio kamili katika uumbaji na usawazishaji (balance), hilo huwaongoza kwenye hitimisho kwamba lazima kuwe na Muumba, ambaye lazima awe ndiye aliyeumba vitu vyote, hivyo lazima kuwe na uwajibikaji.

Wakati aya hizi zilipofunuliwa, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) alisema: "Adhabu imshukie yule anayezisoma bila ya kuzingatia..." – akimaanisha kwamba aya hizi ni lazima zisomwe na kueleweka vizuri.

Ni kwa msingi huu ndipo Imam Hasan al–Basri (Allah amrehemu) alisema: "Kutafakari kwa saa moja ni bora zaidi kuliko kusimama usiku kucha kwa ibada (Qiyamu Llayl)." Kwa hiyo tunaweza kutafakari nini?

Mosi, tunaweza kutafakari majina ya Mwenyezi Mungu ambayo hupatikana mwishoni mwa aya nyingi za Qur'an. Majina haya yanatuongoza kwenye uelewa sahihi wa uhusiano wetu na Muumba wetu, na pia hutumika kama kitovu cha kufinyanga tabia zetu wenyewe.

Pili, tunaweza kutafakari uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Aya tofauti zinatukumbusha tena na tena kutumia macho, masikio na mioyo yetu kutafakari ulimwengu mzima unaotuzunguka, kuelewa madhumuni ya kuumbwa kwetu na kumtambua Muumba wetu.

Katika surat al–Furqan, waja wa Mwenyezi Mungu wametajwa kama, "Na wale ambao wanapokumbushwa Ishara za Mola wao hawajifanyi viziwi nazo, na vipofu." [Qur'an, 25:73].

Tatu, tunaweza kutafakari kuhusu historia ya wanadamu, jinsi madola yenye nguvu yaliyotawala dunia kwa karne nyingi, lakini hatimaye yalianguka na kuacha magofu. Wafalme na Malkia wao waliojitangaza kuwa miungu, vyeo vyao havikuwasaidia kitu na hatimaye waliangamia: "Na Akhera ni bora kwa wamchao Mwenyezi Mungu. Basi hamtafakari?" [Qur'an, 12:109].

Nne, tunaweza kutafakari kuhusu nafsi zetu na jamii yetu. Katika Surat Rum, makafiri wanaulizwa: "Je, hawajifikirii nafsi zao?" Kuna mengi ya kujifunza kutokana na historia, tamaduni na siasa za jamii, ambayo yanatuambia kuhusu mwelekeo wa maadili ya watu na ni nani wanaowachukulia kama miungu. Kuna mengi tunayoweza kujifunza kutokana na jinsi tunavyotendeana, na nini hasa kinachowapa watu hamasa leo.

Mwisho, tunapaswa kukumbuka kifo mara kwa mara. Hili si kwa ajili ya kuhuzunisha balI kutuwezesha kujiandaa kwa ajili ya maisha yetu ya milele yajayo. Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Mwenye akili zaidi ni yule anayekumbuka kifo mara nyingi." [Ibn Majah].

Na Abeid Othman Poyo
0754 990 083

# Washindi mashindano ya Qur'an wanatumikaje kusaidia umma?

Katika miaka ya hivi karibuni, tumeona ongezeko kubwa la mashindano ya Qur'an katika jamii ya Kiislamu. Mashindano haya yanahusisha kuhifadhi Qur'an (Hifdh], tajwid, na usomaji mzuri wa Qur'an.

Kila mwaka katika misikiti, madrasa na taasisi mbalimbali za Kiislamu tunashuhudia watoto, vijana na hata watu wazima wakishiriki katika mashindano haya.

Hili ni jambo jema na la kupongezwa sana kwa sababu linaonyesha mapenzi ya Waislamu kwa Kitabu cha Mwenyezi Mungu.

Qur'an Tukufu ni mwongozo wa maisha ya mwanadamu. Ndiyo sababu Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani] alihimiza sana Waislamu kujifunza na kufundisha Qur'an.

Mtume amesema: "Mbora wenu ni yule anayejifunza Qur'an na akaifundisha." [Bukhari]. Kauli hii ya Mtume inaonyesha wazi kuwa kujifunza Qur'an si jambo la mtu binafsi tu bali ni jukumu linalopaswa kuwanufaisha wengine katika jamii.

Kutokana na msukumo huo, wazazi wengi leo wanapeleka watoto wao madrasa ili wahifadhi Qur'an na wajifunze tajwid.

Pia taasisi mbalimbali zimeanzisha mashindano ya Qur'an kwa lengo la kuwahamasisha watoto na vijana kupenda Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Katika mashindano haya washindi hupata zawadi, vyeti na heshima kubwa katika jamii. Bila shaka hili ni jambo la kutia moyo na linalostahili pongezi.

Hata hivyo, swali muhimu linabaki: baada ya hawa watoto au vijana kushinda mashindano ya Qur'an, wanakwenda wapi? Vipaji vyao vinatumikaje kusaidia umma wa Kiislamu na nchi kwa ujumla? Hili ni swali ambalo jamii inapaswa kulifikiria kwa kina.

## Tuwatumie hivi

Kwanza, washindi wa mashindano ya Qur'an wanaweza kuwa walimu bora wa Qur'an katika jamii. Mtu aliyefanikiwa kuhifadhi Qur'an au kusoma kwa tajwid sahihi ana uwezo mkubwa wa kuwafundisha wengine.

Ikiwa vipaji vyao vitatumiwa vizuri, wanaweza kufungua madrasa au kufundisha katika misikiti na taasisi za elimu. Hivyo watachangia kueneza elimu ya Qur'an na kukuza kizazi kinachoheshimu maadili ya Kiislamu.

Pili, washindi hawa wanaweza kuwa viongozi wa kidini katika jamii. Wengi wao wanaweza kuwa maimamu, makhatibu au wasomaji wa Qur'an katika misikiti.

Uwezo wao wa kusoma Qur'an kwa usahihi unaweza kuwasaidia Waislamu wengi katika ibada zao. Zaidi ya hayo, wanaweza kutoa mawaidha na kuhamasisha watu kuishi kwa kufuata mafundisho ya Qur'an.

Tatu, vipaji vya washindi wa Qur'an vinaweza kusaidia katika kuimarisha maadili ya jamii. Qur'an inafundisha haki, uadilifu, huruma na amani. Watu waliokulia katika mazingira ya Qur'an mara nyingi huwa na maadili mema na hofu ya Mwenyezi Mungu.

Hivyo wakipewa nafasi katika jamii wanaweza kuwa mfano mzuri kwa vijana wengine na kusaidia kupunguza matatizo kama uhalifu, rushwa na mmomonyoko wa maadili.

Nne, washindi wa mashindano ya Qur'an wanaweza kuwa mabalozi wazuri wa Uislamu katika ngazi ya taifa na kimataifa. Katika baadhi ya nchi kuna mashindano ya kimataifa ya Qur'an ambapo washindi wanaiwakilisha nchi yao. Hii inaongeza heshima ya taifa na pia inaonyesha uzuri wa Uislamu kwa dunia. Vijana wenye vipaji vya Qur'an wanaweza kuiwakilisha nchi kwa heshima kubwa.

Hata hivyo, ili vipaji hivi vitumike ipasavyo, jamii na taasisi za Kiislamu zinapaswa kuweka mikakati ya kuwasaidia washindi hawa. Kwa mfano, wanaweza kupewa ufadhili wa masomo ya juu ya elimu ya Kiislamu ili waweze kuongeza ujuzi wao. Pia wanaweza kupewa ajira katika taasisi za dini, madrasa na misikiti.



Serikali na taasisi za elimu pia zinaweza kushirikiana na viongozi wa dini kuhakikisha kuwa vijana hawa wanapata fursa za maendeleo. Hii itasaidia kuhakikisha kuwa vipaji vyao havipotei baada ya mashindano kumalizika.

Kwa upande mwingine, wazazi na jamii wanapaswa kuendelea kuwahamasisha watoto kujifunza Qur'an lakini pia kuwalea katika misingi ya elimu pana. Hifadhi ya Qur'an isiwe mwisho wa safari yao ya elimu bali iwe mwanzo wa kujenga maisha yenye manufaa kwa jamii.

Ikiwa jamii itawaunga mkono, kuwalea na kuwapa fursa washindi wa Qur'an na washiriki kwa ujumla, basi watakuwa hazina kubwa kwa jamii. Watakuwa walimu, viongozi na mabalozi wa maadili mema yanayotokana na Qur'an. Hatimaye, mchango wao utaisaidia jamii kuishi kwa amani, uadilifu na maendeleo yanayolingana na mafundisho ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu.

**MAKALA**
**MAALUM**


Na Said Rajab
0783 650 803

**Akihuzunishwa na uovu na ukosefu wa maadili uliozunguka jamii yake, anajikuta akijitenga na watu wa ukoo wake, akihitaji zaidi na zaidi kuwa peke yake. Akipanda milima inayozunguka mji wake, anaingia kwenye pango dogo. Kutokea hapo, bado anaweza kuiona Nyumba ya Mwenyezi Mungu iliyoyengwa na babu yake, Imam wa tauhid, Nabii Ibrahim (amani ya Allah imshukie).**



# Mambo 10 ya kuzingatia kumi la mwisho la Ramadhan

# Mambo 10 ya kuzingatia kumi la mwisho la Ramadhan



Akihuzunishwa na uovu na ukosefu wa maadili uliozunguka jamii yake, anajikuta akijitenga na watu wa ukoo wake, akihitaji zaidi na zaidi kuwa peke yake. Akipanda milima inayozunguka mji wake, anaingia kwenye pango dogo. Kutokea hapo, bado anaweza kuiona Nyumba ya Mwenyezi Mungu iliyoyengwa na babu yake, Imam wa tauhid, Nabii Ibrahim (amani ya Allah imshukie).

Anachukua chakula pamoja naye, na anatumia siku kadhaa akiwa amejitenga ndani ya pango hili, akiakisi, akitafakari na kufanya ibada. Kisha usiku mmoja kila kitu kinabadilika. Ule utulivu na ukimya wa usiku ule mara unaingiliwa na neno moja, "Soma!"

Mwanadamu mkuu zaidi, kwa mara ya kwanza kabisa anakutana na mkuu wa Malaika wote! Huo ndiyo mwanzo wa zawadi kubwa zaidi ya Allah 'Azza Wajallah' kwa wanadamu. Maneno yake mwenyewe na maneno ya muongozo wa milele yakiwaelekeza watu jinsi ya kuishi na kustawi.

Usiku huu ulibadili mkondo mzima wa historia. Ulimwengu haukuwa tena kama ulivyokuwa awali. Zaidi ya miaka 1,000 baadaye, tunaadhimisha usiku huu wa ajabu. Ni mama wa usiku wote (all nights), usiku wa baraka na msamaha, usiku wa ukuruba na ukaribu zaidi wa mtu na Muumba wake.

Kutokana na mapenzi yake makubwa na ukarimu, Allah 'al–Akram' (Mkarimu) ameupa jina usiku huu kwa ajili yetu 'Laylatul Qadri', na akateremsha sura nzima kwa heshima yake. Sura hii imefunuliwa ili kamwe tusisahau utukufu wa usiku huu, ukubwa wa zawadi hii (Qur'an Tukufu), ukuu wa malaika Jibril aliyehusika na upokeaji wake, ukuu wa Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani zimshukie), ambaye katika moyo wake ndiyo Kitabu hiki kilifunuliwa, na hatimaye ukuu wa Mkuu kuliko wote, Allah Aliyetukuka!

## Ongeza bidii siku 10 za mwisho

Mama Aisha (Allah amridhie) amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akichanganya sala na kulala (usiku) katika siku 20 za mwanzo (za Ramadhan). Lakini zinapokuja siku 10 za mwisho alijikita zaidi katika ibada na kujiweka mbali na wakeze." [Ahmad].

Siku 10 za mwisho wa Ramadhan ni kwa ajili ya ibada ya kina. Kama vile Mtume wa Mwenyezi Mungu alivyojiweka mbali na watu na kufanya itikafu msikitini, sisi pia tunapaswa kujaribu kufanya hivyo. Tunapaswa kupunguza siku nyingi za kazi kadri inavyowezekana na kutumia kipindi hiki kujikurubisha zaidi kwa Allah 'Azza Wajallah'.

Tunapaswa kuepuka kupoteza muda huu wenye thamani kubwa kufanya maandalizi ya Idd, na tujiondoe kabisa katika mitandao ya kijamii. Tunapaswa pia kupigania ustawi wa kiroho na kuimarisha imani katika familia zetu.

Hali ya nyumba zetu, hususan katika usiku wa Ramadhan inapaswa kuwa tofauti na siku nyingine. Mama Aisha (Allah amridhie) amesema: "Kila zilipofika siku 10 za (mwisho wa) Ramadhan, Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akifunga mkwiji wake, (akikaa mbali na wakeze/akijipinda) katika ibada usiku, na aliiamsha familia yake (kwa ajili ya kufanya ibada)." [Bukhari].

Hivyo basi, ni vema Muislamu ukazima mitandao ya kijamii na kuepuka kujivinjari kwenye intaneti katika kumi la mwisho wa Ramadhan. Usipoteze muda kwa ajili ya maandalizi ya Idd. Toa sadaka kila siku na jilazimishe kumuabudu Mwenyezi Mungu. Fanya itikafu na uswali angalau sala ya Isha na Alfajiri kwa jamaa.

Swali sala za usiku (Qiyam Layl) na mara kwa mara muombe Mwenyezi Mungu msamaha na akuepushe na adhabu ya Moto. Pia, jitahidi katika kila usiku kusoma dua zilizosuniwa kadri uwezavyo. Oga vizuri, jipake manukato na jipambe kwa ajili ya usiku huu Mtukufu.

Amesema Imam Ibn al–Jawzi: "Farasi wa mbio anapojua kwamba anakaribia mstari wa mwisho huweka juhudi zote ili kushinda mbio hizo. Usiruhusu farasi wa mbio awe mjanja zaidi kuliko wewe. Hakika, matendo huhukumiwa kutokana na mwisho wake. Kwa hiyo, iwapo hukufanya vizuri wakati wa kuikaribisha Ramadhan, basi huenda ukafanya vizuri wakati wa kuiaga."

*Itaendelea katika toleo lijalo Insha Allah*




SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# KUMI LA PILI:
# Ni fursa ya kujitathmini na kuongeza juhudi

**Muda unaenda kwa kasi ya ajabu. Juzi tu tulikuwa tukisubiri kwa shauku kubwa kuwasili kwa Ramadhan, tukijiandaa kwa ibada, dua na toba. Leo hii tayari tumeiaga theluthi ya mwezi huu mtukufu. Hakika theluthi si haba.**

Hali hii inatukumbusha ukweli mkubwa: umri wetu unaenda haraka, na siku zetu zinapita kwa kasi bila kurudi. Mwenye busara ni yule anayesimama kidogo na kujiuliza, "Nimeitumiaje sehemu iliyopita ya Ramadhan? Nimepiga hatua au nimesimama pale pale?"


Mwenyezi Mungu ametukumbusha katika Qur'an kuwa siku za Ramadhan ni chache mno na zenye kuhesabika. Amesema katika Qur'an, Suratul-Baqarah aya ya 184, yaani: "(Ni) siku chache mno zinazohesabika." [Qur'an, 2:184]. Maneno haya yanatufundisha kuwa siku za mwezi wa Ramadhan si ndefu kama tunavyodhani. Ni siku chache tu, na zinapita kwa haraka. Hivyo, kila siku inapomalizika ni sehemu ya hazina ya fursa inayopungua.

Siku kumi za kumi la pili ni hatua muhimu katika safari ya Ramadhan. Ni kipindi cha kujitathmini na kurekebisha mwelekeo. Aliyetumia siku za mwanzo kwa bidii katika kuswali, kusoma Qur'an, kutoa sadaka na kufanya mema, basi amshukuru Mwenyezi Mungu na aongeze juhudi. Kushukuru si kwa maneno pekee, bali ni kwa kuendelea na ibada kwa uthabiti zaidi. Maana ishara ya kukubaliwa kwa amali njema ni kufuatiwa na amali njema nyingine.

Ama yule aliyepunguza au kuzembea katika siku za mwanzo, basi asikate tamaa. Bado fursa ipo. Ramadhan haijaisha, na milango ya rehema bado iko wazi. Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe na hupenda waja Wake warejee Kwake.

Hili kumi la kati linaweza kuwa mwanzo mpya wa mja kurekebisha uhusiano wake na Mola wake. Hakuna aliyechelewa maadamu bado pumzi ipo na jua halijazama katika maisha yake.

Katika kuhimiza umuhimu wa hatua hizi za Ramadhan, mwanazuoni mashuhuri Sheikh Muhammad ibn Swalih al-Uthaymin (Allah amrehemu) alieleza kuwa siku kumi za kati ni bora kuliko siku kumi za mwanzo, na siku kumi za mwisho ni bora kuliko siku kumi za kati. Hii ni kanuni inayojirudia katika nyakati zenye fadhila: mara nyingi mwisho wake huwa na ubora zaidi kuliko mwanzo wake. Mfano wake ni siku ya Ijumaa, ambapo alasiri yake ina fadhila zaidi; na siku ya Arafah, ambapo sehemu ya mwisho wa siku huwa na ubora mkubwa zaidi.



Hikima ya jambo hili, kama walivyobainisha wanazuoni, ni kwamba nafsi za binadamu zinapoanza kazi ya ibada huwa na hamasa kubwa mwanzoni, lakini baadaye hupata uchovu na kulegea. Hivyo, kuwekwa kwa fadhila kubwa katika nyakati za mwisho ni motisha ili nafsi ijikaze, ijitie nguvu na isilegee njiani. Ni kama msafiri anayeona dalili za kufika mwisho wa safari yake, basi huongeza mwendo ili afike salama.

Ukweli ni kwamba Ramadhan ni safari. Safari hii ina maandalizi, ina juhudi na ina mwisho wake. Maandalizi yetu ni machache, safari ni ndefu, na kituo cha mwisho ni Siku ya Kiyama. Huko hakuna nafasi ya kurejea duniani kuongeza amali.

Aidha, matokeo yake ni mawili tu: Pepo au Moto. Qur'an inasema wazi kuwa watu watagawanyika katika makundi mawili tofauti. Hivyo, mwenye akili hawezi kuchezea siku hizi chache zinazohesabika kwa upuuzi, starehe zisizo na faida, au kujiingiza katika maasi yanayomghadhibisha Mwenyezi Mungu.

Ni heri iliyoje kwa yule atakayezitumia siku hizi katika kumtii Mwingi wa rehema, akapata radhi Zake na kuandikwa miongoni mwa watu wa Peponi. Na ni hasara iliyoje kwa yule atakayeziharibu kwa michezo, uzembe na kumtii shetani, kisha akajikuta amekosa rehema za Mola wake.

Basi, tujifunge mkanda upya katika hizi siku kumi za kati. Tuongeze muda wa kusoma Qur'an, tusimamishe swala kwa khushuu, tutoe sadaka kwa ikhlasi, na tuombe msamaha kwa unyenyekevu. Tusiangalie yaliyopita kwa huzuni isiyo na matokeo, bali tuyatumie kama somo la kutusukuma mbele.

Ramadhan ni chuo cha malezi ya nafsi. Na hizi siku za kati ni mtihani wa kati unaoamua tutafika vipi katika siku kumi za mwisho, ambazo ndizo zenye kilele cha fadhila. Mwenye busara ni yule anayezitumia vizuri siku hizi chache zinazohesabika, ili amalize Ramadhan akiwa karibu zaidi na Mola wake kuliko alivyoanza.

# فتاوى رمضان



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

## Swali: Je, inaruhusiwa kwa mume kumwingilia mkewe katika usiku wa Ramadhan?

**Jibu:** Ndiyo, inajuzu kwa mume kumwingilia mkewe katika usiku wa Ramadhan, na ruhusa hiyo huendelea hadi adhana ya Alfajiri ya pili (adhana ya Swala ya Alfajiri). Hapo mwanzo funga ya Ramadhan ilipoamrishwa, jambo hili lilikuwa limekatazwa, kama ilivyothibiti katika hadith kutoka kwa Al-Baraa (Allah amridhie).

Al-Baraa amesema: "Ilipofaradhishwa saumu ya Ramadhan, walikuwa hawawakaribii wake zao katika Ramadhan yote, na baadhi ya wanaume walikuwa wakijikhini nafsi zao (yaani wakivunja katazo hilo kwa siri). Hapo Allah akateremsha: 'Allah anajua kwamba mlikuwa mkizikhini nafsi zenu, basi Amewakubalikieni toba na Amekusameheni...'" [Qur'an, 2:187]. [Bukhari]

Imamu Al-Bukhari katika Sahihi yake ameweka mlango kuhusu kauli ya Allah Mtukufu: "Mmehalalishiwa usiku wa saumu kuwaendea wake zenu; wao ni vazi kwenu nanyi ni vazi kwao. Allah anajua kwamba mlikuwa mkizikhini nafsi zenu, basi Amewakubalikieni toba na Amekusameheni. Basi sasa waendeeni na tafuteni alichokuandikieni Allah..." [Qur'an, 2:187].

Kutoka kwa Al-Baraa (Allah amridhie) amesema: "ilikuwa Swahaba wa Mtume (Allah amshushie rehema na amani) mtu akiwa amefunga, muda wa kufuturu ukifika kisha akalala kabla hajala, basi hakuwa akila usiku huo wala mchana unaofuata mpaka jioni.

Hivyo, Qays bin Sirmah Al-Ansari alikuwa amefunga na wakati wa kufuturu ulipofika alimwendea mke wake na kumwambia: 'Je, una chakula?' Akasema: 'Hapana, lakini nitaenda kukutafutia.' Alikuwa amechoka kwa kazi ya mchana, usingizi ukamshinda. Mke wake aliporudi akamkuta amelala. Alipomwona akasema: 'Hasara kwako!' Ilipofika katikati ya mchana akazimia.

Tukio hilo likamfikia Mtume (Allah amshushie rehema na amani), ndipo ikateremshwa aya: 'Mmehalalishiwa usiku wa saumu kuwaendea wake zenu...' Maswahaba wakafurahi sana kwa aya hiyo. Na pia ikateremshwa: 'Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu uzi mweupe kutokana na uzi mweusi (yaani mapambazuko)...'" [Qur'an, 2:187]. [Bukhari]

Al-Hafidh Ibn Hajar ameeleza kuwa riwaya zote zinakubaliana kwamba mwanzoni katazo lilihusishwa na kulala; mtu akilala baada ya kufuturu (au baada ya muda wa kufuturu kuingia) kabla hajala au kabla ya kumwingilia mkewe, basi hakuruhusiwa kula, kunywa wala kumwingilia hadi siku inayofuata jioni.

Baadhi ya riwaya zimehusisha katazo hilo na Swala ya 'Isha, kwa kuwa baada yake mara nyingi watu hulala. Lakini maana ya msingi ilikuwa ni kulala. Imeelezwa pia kuwa hukumu hiyo ya awali ilikuwa sawa na ilivyokuwa kwa Ahlul-Kitab (Watu wa Kitabu). Imepokewa katika Sahihi Muslim kwamba Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Tofauti kati ya saumu yetu na saumu ya Watu wa Kitabu ni kula daku (sahur)." [Muslim]

Imamu Al-Qurtubiy katika tafsiri yake amesema kuwa neno "Mmehalalishiwa" linaonesha kwamba jambo hilo lilikuwa limeharamishwa hapo kabla, kisha likafutwa.

Imepokewa kwamba 'Umar (Allah amridhie) aliwahi kumwingilia mke wake baada ya kulala, kisha akaja kwa Mtume (Allah amshushie rehema na amani) akiomba udhuru. Hapo Allah akateremsha aya: "Allah anajua kwamba mlikuwa mkizikhini nafsi zenu, basi Amewakubalikieni toba na Amekusameheni. Basi sasa waendeeni..." [Qur'an, 2:187].

Kwa ufupi, inajuzu kwa mwanaume kumwingilia mke wake katika usiku wa Ramadhan hadi adhana ya Alfajiri. Katazo lililokuwepo mwanzoni lilifutwa, na uhalali wake umethibiti wazi katika Kitabu cha Allah (Qur'an). Na Allah ndiye Mjuzi Zaidi.

## Swali: Ni ipi tofauti kati ya fidia na kafara katika saumu, na kila moja hulazimu lini?

**Jibu:** Watu wengi huchanganyikiwa kuhusu tofauti kati ya fidia na kafara katika saumu. Tofauti yake ni kama ifuatavyo:

Kwanza: Fidia. Fidia imetajwa katika kauli ya Mwenyezi Mungu: "Na wale wanaoiweza (kwa shida) watalipa fidia ya kumlisha maskini. Na atakayefanya wema zaidi basi ni kheri kwake. Na kufunga ni bora kwenu ikiwa mnajua." [Qur'an, 2:184]. Aya hii inamhusu mzee kikongwe na aliye katika hali kama yake ambaye hawezi kufunga. Huyu anaruhusiwa kufungua na kwa kila siku aliyofungua atoe fidia ya kumlisha maskini mmoja.

Wanaofanana na mzee huyo ni ajuza (mwanamke mzee dhaifu sana), pamoja na mgonjwa wa maradhi sugu yasiyotarajiwa kupona. Baadhi ya wanazuoni wamemjumuisha pia mwanamke mjamzito na anayenyonyesha ikiwa ana hofu kwa mtoto wake, wakisema alipe fidia na alipe pia qadha. Lakini kauli yenye nguvu zaidi ni kuwa mjamzito na anayenyonyesha wanatakiwa kulipa qadha tu bila fidia.

Pia, wanazuoni wengi wanasema kuwa mwenye deni la qadha ya Ramadhan akachelewesha hadi Ramadhan inayofuata bila udhuru, basi atalipa qadha pamoja na fidia. Lakini madhehebu ya Hanafi wanasema analazimika qadha tu bila fidia, na hii ndiyo kauli yenye nguvu zaidi kwao.

Kiasi cha fidia ni mudd (kibaba) kimoja kwa kila siku. Mudd ni kipimo cha Mtume (Allah amshushie rehema na amani), ambacho kwa zama hizi ni takriban nusu kilo au

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
+255 789 201383

# Tuzingatie makusudio ya Qur'an tunapohudhuria mashindano

Tangu kuanza kwa mwezi Mtukufu wa Ramadhan tumeshuhudia mashindano mbalimbali ya kusoma na kuhifadhi Qur'an tukufu, yenye hadhi ya Kitaifa na Kimataifa. Kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, mashindano yote ya mwaka huu yamehudhuriwa na idadi kubwa ya watu kutoka ndani na nje ya Tanzania huku wengine wakiyafuatilia kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Kwa zaidi ya miaka mitano sasa, mashindano hayo ya kusoma na kuhifadhi Qur'an yamekuwa yakileta msisimko wa kipekee unaochagizwa na zawadi za washindi pamoja na umahiri wa wasomaji wanaoshindana. Maelfu ya watu humiminika viwanjani na katika kumbi mbalimbali kushuhudia mashindano hayo, jambo ambalo pia huongeza msisimko.

Idadi kubwa ya watu (Waislamu na wasio Waislamu) wanaojitokeza katika mashindano hayo kila mwaka inaonesha namna Qur'an inavyomgusa kila binadamu. Swali la msingi la kujiuliza ni je, tunapohudhuria mashindano ya Qur'an kila mwaka tunazingatia makusudio na malengo ya kuteremshwa kwa Kitabu hicho Kitukufu?

Bila shaka jibu la walio wengi ni hapana! Hali hii inatupa taswira ya kuwapo kundi kubwa la Waislamu wasiofahamu tafsiri ya maneno ya Qur'an. Kinachoonekana ni wahudhuriaji wengi wa mashindano ya Qur'an kuwashangilia wasomaji wenye sauti nzuri pasina kuelewa maana/ tafsiri ya kile kinachosomwa.

Hili haliko sawa hata kidogo, lakini pengine linajitokeza kwa sababu ya kutofanya juhudi ya kujifunza Qur'an na kuelewa maana yake. Waislamu wengi hatuijui Qur'an na hata inapoingia Ramadhan tunakuwa wavivu wa kuhudhuria darsa.

Tumeifanya Ramadhan kama msimu wa kulala na kupoteza muda katika michezo ya pumbao. Allah Mtukufu anasema: "Na Mtume atasema (Siku ya Kiyama), 'Ewe Allah, hakika watu wangu waliifanya hii Qur'an kitu kilichohamwa.'" [Qur'an, 25:30]. Haya ni matokeo ya kutoipa hadhi na thamani inayostahili Qur'an.

Kimsingi, suala la kujifunza Qur'an na kuelewa maana yake limekosa thamani katika zama tulizonazo, licha ya Masheikh kulisisitiza mara kwa mara. Waislamu wengi hawahudhurii darsa za mafunzo ya Qur' an kwa kisingizio cha kutingwa na majukumu ya kikazi. Kadhalika, kuna wanaoona hawawezi tena kujifunza na kuielewa Qur' an kwa sababu tu wana umri mkubwa (watu uzima).

Haya yote yanatokana na dhana potofu ya baadhi ya Waislamu katika kufahamu maana ya ibada. Baadhi ya Waislamu wanainasibisha ibada ya Allah na matendo maalumu ya sala, zaka, funga, hijja na ibada nyingine za Sunna. Kwa dhana yao hiyo, huyaona matendo yote yaliyo nje ya sala, zaka, swaumu na mengineyo kuwa si katika ibada.

Huu ni mtazamo potofu uliojengeka kwenye vichwa vya Waislamu wengi. Endapo dhana hii itaendelea kudumu katika fikra za Waislamu, basi hakuna shaka suala la ibada litazingwa ndani ya wigo maalum. Hii ni kinyume na lengo la mwanzo la wahyi (ufunuo) linalomtaka mwanadamu kushikamana na suala la kutafuta elimu.

Ukweli mchungu ni kwamba, wengi wetu tunaihama Qur'an mwaka mzima na kuikumbuka mwezi wa Ramadhan tu au wakati wa kuzika wafu wetu, jambo ambalo ni kinyume na maelekezo ya dini. Tukumbuke kwamba Waislamu ndiyo walengwa wa kwanza wa Qur' an, hivyo tunawajibika kujifunza na kuelewa maana yake, hususan katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan.

Kwa kufanya hivyo tutamfahamu Allah kisawasawa na kumuabudu ipasavyo. Kuisoma Qur'an ni ibada na maneno yake ni maneno yenye hadhi na utukufu wa kipekee, hivyo Muislamu anaposhindwa kuisoma na kuifanyia kazi anakuwa amekwenda kinyume na malengo ya dini.





MAKALA MAALUM

UKHTI FATIMA SS

# Ramadhan na alama yake ya kiuchumi

Kadiri mwezi mtukufu wa Ramadhan unavyoendelea nchini Tanzania, mabadiliko yanaonekana wazi—sio tu katika maisha ya kiroho ya Waislamu, bali pia katika mwenendo wa uchumi.

Masoko ya iftar yanapochangamka, biashara za vyakula zinaongezeka, na matumizi ya kaya hupanda, Ramadhan huacha kile ambacho wachambuzi wa uchumi wanaweza kukiita alama yake ya kiuchumi—mchanganyiko wa ibada, matumizi na shughuli za kijamii zinazoathiri mwenendo wa soko.

Kwa mtazamo wa juu juu, Ramadhan ni mwezi wa kujizuia na ibada. Lakini katika uchumi wa nchi zenye idadi kubwa ya Waislamu kama Tanzania, ni pia kipindi cha shughuli kubwa za kiuchumi.

Mahitaji ya bidhaa kama vyakula vya iftar, tende, vinywaji, nafaka, mavazi ya Eid na zawadi huongezeka kwa kasi. Hali hii husababisha biashara ndogo ndogo—hasa za chakula na mavazi—kustawi kwa muda mfupi lakini wenye athari kubwa.

Mabadiliko haya ya tabia ya matumizi yanaendana na kile ambacho wataalamu wa uchumi wa halal wanaita "Ramadan economic signature"—yaani muundo maalumu wa matumizi na uhamishaji wa fedha unaojitokeza kila mwaka katika mwezi huo.

Sehemu muhimu ya alama hiyo ni utoaji wa sadaka na Zakat. Kwa mujibu wa mafundisho ya Kiislamu, Waislamu wenye uwezo wanatakiwa kutoa asilimia 2.5 ya akiba yao kama Zakat. Kwa pamoja na sadaka nyinginezo zinazotolewa wakati wa Ramadhani, utaratibu huu husababisha mtiririko mkubwa wa fedha kutoka kwa wenye uwezo kwenda kwa wahitaji. Katika mantiki ya kiuchumi, huu ni mfumo wa ndani wa usambazaji wa utajiri unaochochea matumizi katika ngazi za chini za jamii.

Katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Tanga na Zanzibar, athari hizi zinaonekana wazi. Biashara za iftar, wauzaji wa tende, mikate, juisi, na vyakula vya jadi hupata wateja wengi zaidi kuliko miezi mingine.

Wafanyabiashara wa mitandaoni pia hunufaika, hasa kupitia mitandao ya kijamii kama WhatsApp, Instagram na Facebook ambako bidhaa za vyakula, manukato, mavazi ya staha na zawadi za Eid hutangazwa kwa wingi.

Kwa vijana wa Tanzania, hasa wale wanaotumia teknolojia, Ramadhan inaweza kuwa si tu mwezi wa ibada bali pia maabara ya ujasiriamali. Kutoka huduma za iftar zinazotumwa majumbani, hadi biashara za bidhaa za Sunnah kama asali, habbatus-sauda na bidhaa za asili, soko linalohusishwa na mtindo wa maisha wa Kiislamu linaendelea kukua.

Kwa mtazamo mpana, Ramadhan inaonyesha jinsi imani, jamii na uchumi vinavyoweza kuungana. Changamoto zinazojitokeza kila mwaka—kuanzia bei za vyakula hadi upatikanaji wa bidhaa—zinaweza pia kuwa fursa za ubunifu kwa wafanyabiashara na wajasiriamali. Kwa hiyo, Ramadhan si mwezi wa kiroho tu. Ni pia injini ndogo lakini yenye nguvu ya uchumi—na kwa vijana wa Tanzania wenye mawazo ya biashara, inaweza kuwa mwanzo wa fursa mpya.



Na Abeid Othman Poyo
0754 990 083

# Mwezi wa kuchuma thawabu unapogeuka wa kula

Mwezi mtukufu wa Ramadhan ni msimu wa kipekee katika maisha ya Muislamu. Ni mwezi wa rehema, msamaha na kuachwa huru na moto na ambao ndani yake iliteremshwa Qur'an Tukufu. "Mwezi wa Ramadhan ambao imeteremshwa humo Qur'ani kuwa ni uwongofu kwa watu na hoja zilizo wazi za uongofu na upambanuzi..." [Qur'an, 2: 185].

Kwa hakika, huu ni mwezi wa kuchuma thawabu, mabadiliko ya tabia, uchamungu na radhi za Mola. Lakini kwa masikitiko makubwa, katika jamii zetu nyingi, mwezi huu, leo, umegeuka kuwa mwezi wa kula na shindano la meza zenye vyakula vya kila aina.

Masoko hujaa pilikapilika, bei hupanda, watu hujaza mafriji na makabati kana kwamba wanaandaa karamu ya kila siku. Hali hii inatutaka tusimame na kujiuliza: Je, kweli huu ndio ulikuwa ujumbe wa Ramadhan?



## Lengo la Saumu ni kukuza uchamungu

Mwenyezi Mungu ameeleza wazi lengo la kufaradhishwa saumu katika kauli Yake: "Enyi mlioamini! Mmefaradhishiwa saumu kama ilivyofaradhishwa kwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kuwa wachamungu." [Qur'an, 2: 183].

Aya hii inabeba hekima kubwa. Lengo si njaa wala kiu pekee, bali ni kufikia daraja ya taqwa yaani uchamungu unaomfanya mja awe makini katika matendo yake, maneno yake na fikra zake.

Saumu ni madrasa ya malezi ya nafsi. Inamfundisha Muislamu subira, nidhamu, kujizuia na huruma. Mtu anapohisi njaa na kiu, anakumbuka hali ya wahitaji wanaoishi maisha ya upungufu kila siku.

Saumu inakusudiwa kuamsha dhamira ya kusaidiana, kuhurumiana na kugawana kile alichonacho mtu.

Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani] alisisitiza umuhimu wa maadili katika saumu. Katika Hadith mashuhuri amesema: "Asiyeacha uongo basi Mwenyezi Mungu hana haja ya yeye kuacha chakula chake na kinywaji chake."

Hii inaonyesha wazi kuwa saumu si tendo la kimwili pekee, bali ni ibada inayolenga mageuzi ya ndani. Ramadhan ni msimu wa kuzidisha ibada kama kusoma Qur'an, kuswali Tarawehe, kutoa sadaka, kuomba msamaha na kufanya tafakuri ya kina kuhusu maisha yetu. Ni mwezi wa kuanza upya. Ni mwezi wa kuvuna mema yatakayotuongoza miezi mingine kumi na moja.

Hata hivyo, taswira inayoonekana katika sehemu nyingi ni tofauti. Badala ya kuzingatia ibada na tafakuri, nguvu nyingi zinaelekezwa katika maandalizi ya futari zenye gharama kubwa.

Jedwali la vyakula linakuwa refu kuliko orodha ya dua. Kipaumbele kinageuka kutoka kwenye Qur'an na ibada kwenda kwenye mapishi na ununuzi.

## Ramadhan ya fahari na kilio cha wahitaji

Ni jambo la kusikitisha kuona kuwa katika jamii ambamo wapo watu wanaokosa hata mlo mmoja wa kufuturu, wengine wanatumia Ramadhan kama jukwaa la kuonyesha uwezo wa kifedha kupitia vyakula vya fahari.

Picha za meza zilizojaa aina kumi au ishirini za vyakula husambazwa kwa majigambo. Mabaki ya chakula hutupwa kwa wingi, ilhali jirani anaweza kuwa hana hata tende ya kufuturia.

Hii ni kwenda kinyume na roho ya saumu. Ramadhani inapaswa kutukumbusha unyenyekevu na mshikamano wa kijamii. Inapaswa kutuunganisha na maskini, si kututenganisha nao kwa tabaka la meza zetu.

Uislamu haukatazi kula vizuri wala kufurahia neema za Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu amesema: "Kuleni na kunyweni, wala msifanye israfu (kupita kiasi]; hakika Yeye hawapendi wafanyao israfu." [Qur'an, 7:31]. Hapa kuna mizani. Kula na kunywa kunaruhusiwa, lakini pasipo israfu, pasipo kujionyesha, na pasipo kusahau wajibu kwa wengine.

Ramadhan si mwezi wa mateso wala kujinyima kupita kiasi. Si wito wa kuacha kula vizuri kabisa. Hapana. Lakini ni wito wa kuweka mipaka, kuepuka anasa zisizo za lazima, na kukumbuka kuwa neema tulizonazo ni amana. Tunapozidisha matumizi kwa ajili ya fahari, huku tukisahau wahitaji, tunapoteza hekima ya saumu.

Ni wajibu wa kila Muislamu kujiuliza: Je, Ramadhan yangu imenibadilisha? Je, imenifanya niwe mkarimu zaidi? Je, imenifanya nijali zaidi mayatima, wajane na maskini? Kama jibu ni sio basi kuna haja ya kutafakari upya namna tunavyouishi mwezi huu.

Jamii zetu zinaweza kubadilika ikiwa kila mmoja atachukua hatua ndogo. Badala ya kuandaa vyakula vya aina kumi visivyoliwa vyote, tunaweza kupunguza na sehemu ya gharama hiyo tukawapelekea wahitaji.

Badala ya kushindana kwa mapambo ya meza, tushindane kwa kusoma Qur'an na kutoa sadaka. Badala ya fahari ya chakula, tuwe na fahari ya taqwa.

Ramadhan ni uwekezaji wa milele. Ni shamba la kupanda mbegu za Akhera. Mkulima mwenye busara hapandi ili aonekane, bali ili avune. Vivyo hivyo, Muislamu mwenye hekima hatumii Ramadhan kwa maonesho, bali kwa kujijenga kiroho.

Tusikubali mwezi wa kuchuma ugeuke kuwa mwezi wa kula tu. Tuurudishe katika nafasi yake ya asili yaani kuwa mwezi wa malezi, mageuzi na mshikamano.

Tukiifanya Ramadhan kuwa shule ya taqwa, basi tutavuna matunda yake si mwezi mmoja tu, bali katika maisha yetu yote.

NASAHA ZA WIKI

0787 503 085

NA YUSUFU AMINI



# Darsa za Ramadhan na malezi ya kiimani



Kujifunza elimu ya dini ni katika mambo ya msingi yanayomuwezesha Muislamu kujenga uhusiano mwema na Mola wake. Kwa msingi huo, ni juu ya kila muumini kujifunza elimu hiyo ili aweze kutekeleza ibada mbalimbali, ikiwemo sala.

Ili kuufikisha umma kwenye lengo mahsusi la kuumbwa (uchamungu), wanazuoni wa Kiislamu, hususan katika kipindi hiki cha mwezi wa Ramadhan, wanawajibika kuufunza umma Qur'an tukufu ambayo ndiyo msingi wa tauhidi.

Sambamba na hilo, ni vema waumini wakajiwekea lengo katika kuisoma Qur'an pamoja na kuifanyia kazi – jambo ambalo ni mwanzo mzuri wa kumfanya mja kuishi kwa mujibu wa tauhidi, yaani kumpwekesha Mwenyezi Mungu.

Kukosekana kwa elimu hii ya tauhidi kunatajwa na Masheikh pamoja na walinganiaji kuwa ni miongoni mwa sababu za baadhi yetu kushindwa kufikia lengo la Ramadhan (uchamungu), licha ya malezi ya kiimani na kiitikadi yatolewayo kupitia darsa za Ramadhan.

Kukabiliana na hali hii, ipo haja kwa waumini kuisoma Qur'an na kuzingatia mafundisho yake. Kwa hakika katika kulitekeleza hili kuna faida nyingi ndani yake katika maisha haya ya dunia na kesho Akhera. Qur'an yatuambia: "...Allah habadilishi kabisa neema alizowaneemesha watu, mpaka wao wabadilishe yaliyomo ndani ya nafsi zao. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua." [Qur'an, 8:53].

Aya hii tukufu inatuhimiza kufanya mabadiliko ndani ya nafsi zetu. Kuliendea hilo, ni vema darsa za Ramadhan zikatumika katika kuleta mabadiliko ya kitabia na mienendo kwa waumini ili kuwafanya waishi kwa mujibu wa sheria za Kiislamu.

Sanjari na hilo, Masheikh na walinganiaji wanalo jukumu la kuwanasihi Waislamu waliojibunia utamaduni wa kumuabudu Mwenyezi Mungu katika mwezi wa Ramadhan pekee kuacha kufanya hivyo. Waislamu wa aina hii watambue kuwa, Mwenyezi Mungu anastahiki kuabudiwa kila siku na siyo katika misimu maalum.

Kumuabudu Mungu ndani ya Ramadhan peke yake inaweza kuwa dalili ya ushirikina kwa sababu, kufanya hivyo ni sawa na kujaalia uwepo wake ndani ya Ramadhan pekee na kwamba katika miezi mingine hutoweka.

Kuhusiana na hili, Mwenyezi Mungu anatukumbusha akisema: "Enyi mliyoamini! Ingieni katika Uislamu kikamilifu, wala msifuate nyayo za shetani. Hakika yeye (shetani) kwenu ni adui wa wazi." [Qur'an, 2:208].

Bila shaka Allah ameifanya funga kuwa ngome na kinga ya wamchao Yeye dhidi ya shari za nafsi. Kwa msingi huo, tunawajibika kulainisha nyoyo zetu katika kupenda kutekeleza ibada mbalimbali. Walinganiaji wanapaswa kutumia lugha laini pindi wanapowapa nasaha Waislamu wenye desturi ya kufanya ibada ndani ya Ramadhan pekee.

Kufanya hivyo kuna faida zaidi katika kuwashawishi kuendelea na ibada ya sala hata baada ya kumalizika Ramadhan. Ni wazi lengo kuu la kufaradhishwa swaumu ya Ramadhan ni kuwaandaa waja kufikia lengo la uchamungu, ambao ndiyo msingi mkuu wa kuwapo kwao ulimwenguni.

Katika hili, tunaweza kuchukua mfano kwa mfungaji ambaye anatakiwa kujiepusha na dhambi ya kusema uongo. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Yule ambaye hatoacha maneno ya uongo na kuyafanyia kazi, Allah hana haja na yeye kuacha chakula chake na kinywaji chake (yaani Allah hakubali swaumu yake)." [Bukhari].

Hiyo ina maana kuwa, funga ni zoezi mahsusi la kuidhibiti nafsi dhidi ya mambo ya haramu. Kwa hiyo, itakuwa ajabu kwa waumini kushindwa kujizuia na yaliyoharamishwa ambayo hata hivyo hayawezi kuwaletea faida kwenye maisha yao ya duniani wala Akhera.

Ili kujenga mustakbali bora wa maisha yetu ya Akhera, hatuna budi kuishi kwa mujibu wa mifumo iliyowekwa na dini. Siku zote tujiulize; ni njia gani bora ya kutuwezesha kufaidika na Ramadhan?

Swali hili, mara nyingi limekuwa haliwashughulishi watu isipokuwa wenye imani pekee. Hao, wanaoshughulishwa na swali hilo, ndiyo wanaojua fadhila zinazopatikana ndani ya Ramadhan na wakafanya pupa ya kuhakikisha wanafikia lengo huku wakielekeza mategemeo yao kwa Allah Ta'ala.

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Upunjaji mizani: jinai inayohalalishwa kimyakimya katika jamii zetu

## Tatfif: katika uongozi, siasa na utumishi wa umma

**Katika makala zilizotangulia, tumeona jinsi Tatfif (upunjaji) unavyojitokeza kazini, katika ndoa, elimu na biashara. Tumeona namna mtu anavyoweza kupunja muda, wajibu au haki ya mwingine kwa kisingizio cha kawaida kabisa. Lakini upunjaji unapopanda ngazi na kuingia katika uongozi, siasa na utumishi wa umma, madhara yake hayabaki kwa mtu mmoja au familia moja; huathiri maelfu au hata mamilioni ya watu kwa wakati mmoja. Hapa, upunjaji haupimi kilo, mita wala saa; hupima uaminifu, uwajibikaji na dhamira ya kweli ya kutumikia. Ni upunjaji wa mizani ya haki na amana.**

### Mfano wa Qur'an wa uongozi usio na tatfif

Qur'an inatupatia mfano wa uongozi ulio safi usio na upunjaji kupitia kisa cha Nabii Yusuf (amani ya Allah iwe juu yake). Nabii Yusuf alidhihirisha uwezo wake wa kusimamia rasilimali za taifa wakati wa dhiki, alisema: "Niteue juu ya hazina za nchi; hakika mimi ni mlinzi makini mwenye kujua mno." [Qur'an, 12:55].

Katika kauli hii kuna misingi miwili mikuu ya uongozi wa haki: uaminifu (hafidh) wa kulinda amana na maslahi ya watu, na uwezo pamoja na maarifa ('alim) wa kuwa na ujuzi wa kutosha kutekeleza jukumu. Sifa hizi mbili zinapoungana, huzaa uongozi wenye mizani iliyonyooka. Lakini pale mojawapo inapokosekana—iwe ni uaminifu au uwezo—Tatfif huanza polepole. Kiongozi asiye mwaminifu atatumia uwezo wake vibaya; asiye na uwezo, hata akiwa mwaminifu, atasababisha madhara kwa uzembe.

Tatfif katika uongozi hujitokeza pale ambapo nafasi hutafutwa kwa maslahi binafsi badala ya huduma kwa jamii, mamlaka hutumika kwa faida ya wachache badala ya wengi, na uwajibikaji hudaiwa kwa walio chini pekee huku walio juu wakijiona wako juu ya sheria. Huu ni upunjaji wa wazi: kudai heshima, mamlaka na marupurupu, lakini kutotoa huduma, ulinzi na haki kwa wananchi. Ni kuchukua kikamilifu kutoka kwa umma, lakini kurejesha nusu au chini ya hapo.

Katika siasa, Tatfif mara nyingi huvalia sura ya ahadi tamu. Wakati wa kampeni, maneno huwa mengi; baada ya ushindi, vitendo huwa haba. Ahadi hutolewa bila mpango wa utekelezaji, sera huandikwa kwa uzuri kwenye karatasi lakini hubaki dhaifu katika utekelezaji, na kauli za uwazi pamoja na uwajibikaji hutolewa hadharani huku maamuzi yakifanyika gizani.

Wananchi hulishwa matumaini makubwa, lakini matokeo wanayopokea ni madogo. Hii ni Tatfif wa matumaini ya umma, kupunja imani ya watu kwa maneno yasiyo na uzito wa vitendo.

Utumishi wa umma ni amana. Mtumishi wa umma analipwa kwa kodi za wananchi ili awahudumie kwa haki na ufanisi. Lakini Tatfif huonekana pale ambapo huduma zinacheleweshwa makusudi au kwa uzembe, maamuzi yanategemea upendeleo, rushwa au ukaribu badala ya haki, na wananchi huzungushwa kutoka ofisi moja hadi nyingine bila sababu huku mishahara ikiendelea kulipwa.

Hapa mizani inapunjwa kati ya kodi inayokusanywa na huduma inayorejeshwa kwa wananchi. Ni kuchukua haki ya mshahara kamili kwa kazi isiyotekelezwa kikamilifu.

Matokeo ya Tatfif katika uongozi ni mazito na ya muda mrefu. Wananchi hukata tamaa na kupoteza imani kwa viongozi wao, taasisi huporomoka kwa kukosa uadilifu, dhulma na migogoro huimarika kwa sababu haki haionekani kutendeka, na maendeleo ya taifa hudumaa kwa kukosa mwelekeo na usimamizi thabiti.

Zaidi ya yote, jamii inapoona upunjaji unatoka juu bila kuadhibiwa, wa chini nao huiga. Hivyo, Tatfif hugeuka kuwa utamaduni si kosa la mtu mmoja, bali mwenendo wa kitaifa.

Kurekebisha hali hii kunahitaji kurejesha mizani ya maadili. Qur'an inatuonesha kuwa uongozi wa haki hauanzi na vyeo, bali na sifa: uaminifu kabla ya umaarufu, uwezo kabla ya ukaribu au undugu, na uwajibikaji kabla ya mamlaka.

Kiongozi anayekumbuka kuwa atawajibika mbele ya Allah kwa kila uamuzi wake hatothubutu kupunja mizani ya watu wake. Atatambua kuwa mamlaka si fursa ya kujinufaisha, bali ni jukumu zito la kulinda haki.

Tatfif katika uongozi ni hatari kuliko aina nyingine zote, kwa sababu huweka mfano kwa jamii nzima. Mfano unapoharibika uongozi wa juu, athari zake hushuka chini kwa kasi. Na pale kizazi kinapokulia katika mazingira ya kuona upunjaji kama jambo la kawaida, uharibifu wake huwa wa kina na wa muda mrefu.

Mizani ya taifa lolote husimama juu ya uadilifu wa viongozi wake. Ikiwa mizani hiyo itapunjwa, hata juhudi za watu wema zitakuwa na matokeo hafifu. Katika makala inayofuata (ya mwisho), tutachunguza Tatfif katika Imani, Ibada na Nafsi, eneo ambalo Tatfif huanza kimya kimya ndani ya moyo kabla ya kuonekana katika familia, kazi, biashara na hata uongozi. Usikose makala ya mwisho ya mfululizo..

***Usikose makala inayofuata.***

رمضان

**MAKALA MAALUM**

0712 690 811

NA SHEIKH SEIF RUGA



# Adabu za wajibu katika swaumu ya Ramadhan

Wajibu ni tendo ambalo Muislamu akilifanya hulipwa thawabu, na akiliacha hustahiki adhabu. Swaumu ya Ramadhan ina adabu za lazima ambazo ni wajibu kwa mfungaji kuzilinda na kuzitekeleza – iwe za kauli au vitendo. Hivyo basi, mfungaji anatakiwa kushikamana na wajibu wote wakati wa funga na nje ya funga, akiwa nyumbani au safarini.

Mfungaji hapaswi kuacha jambo lolote alililoliwajibisha Allah Mtukufu, na katika wajibu ulio mkubwa zaidi baada ya mtu kutamka shahada mbili ni kusali sala tano. Ingawa kusali ni wajibu wakati wa funga na wakati mwingine wowote, baadhi ya wafungaji hupuuzia wajibu huu wakidhani kuwa hauthiri dini yao wala swaumu yao.

Wapo wanaolala na kuacha sala kwa makusudi, na wanapoamka hawailipi kwa uzembe. Wengine hukesha usiku, hasa katika mwezi wa Ramadhan na hulala muda mfupi kabla ya kuingia Alfajiri, hivyo kupitiliza na kuikosa sala ya Alfajiri. Vilevile, kuna ambao hulala sana mchana na kuamka jioni (karibu na muda wa kufuturu), kisha hushughulika na maandalizi ya futari na daku na kujikuta wanaacha kusali sala ya Magharibi na hata Isha.

Pia, kuna wanaosali sala za faradhi lakini hawasali kwa jamaa msikitini. Ama wale wanaoacha kabisa kusali kwa kupuuzia, wanatakiwa watubu kwa Allah, wajutie kitendo hicho na waanze kusali sala tano za faradhi.

## Hukumu ya mwenye kuacha sala

Kuacha sala ya faradhi kwa kupinga wajibu wake ni ukafiri mkubwa, kwa mujibu wa makubaliano ya pamoja ya wanazuoni. Mwenye kuacha sala kwa kupuuzia huku akiamini kuwa utekelezaji wake ni jambo la wajibu, ataandikiwa madhambi makubwa hivyo anatakiwa atubu na kujuta kwa kitendo chake hicho.


Allah Mtukufu anasema: "Kila nafsi itakuwa (itawekwa) rehani kwa yale iliyoyachuma, isipokuwa watu wa kuliani wakiwa katika Pepo, wataulizana juu ya (watu) waovu: 'Ni nini kilichowapeleka Motoni?' Watasema: 'Hatukuwa miongoni mwa wanaosali, wala hatukuwa tukiwalisha masikini. Na tulikuwa tukizama pamoja na waliozama katika maovu, na tulikuwa tukikanusha Siku ya Malipo.'" [Qur'an, 74:38–46],

Hivyo, mwenye kuacha sala anahesabiwa kuwa miongoni mwa watu waovu watakaoingia Motoni, kama Allah anavyoeleza: "Hakika wakosefu (waovu) wamo katika upotofu na wazimu. Siku watakapokokotwa Motoni kifudifudi waambiwe: Onjeni mguso wa Jahannamu!" [Qur'an, 54:47–48].

## Hukumu ya sala ya jamaa

Wanazuoni wa sharia ya Kiislamu wametofautiana mitazamo yao kuhusu hukumu ya sala ya jamaa. Wapo wanaoona kuwa kuitekeleza ni katika Sunna zilizosisitizwa na wala si jambo la wajibu na lazima, kama ilivyo kwa madhehebu yetu ya Kishafi.

Na kuna wanaoona kuwa kusali sala tano kwa jamaa msikitini ni jambo la lazima (faradhi a'in) kwa kila Muislamu mwanaume aliye mjini au safarini. Hoja ya wenye mtazamo huu imetokana na maelekezo ya Qur'an tukufu, Sunna ya Mtume (rehema na amani zimshukie), na mafundisho ya Masahaba (Allah awaridhie wote).



Allah alimuamuru Mtume wake kutekeleza ibada ya sala kwa jamaa, hata katika mazingira ya vita, aliposema: "Na (Muhammad) utakapokuwa pamoja nao ukawasalisha, basi kundi moja miongoni mwao wasimame pamoja nawe na wachukue silaha zao. Na watakaposujudu wawe nyuma yenu (kuwalinda). Na lije kundi jingine ambalo halikusali, lisali pamoja nawe. Nao washike hadhari yao na silaha zao..." [Qur'an, 4:102].

Aya hii inaonesha kwamba sala ya jamaa ni faradhi inayopasa kutekelezwa na kila mtu mwenyewe (faradhi a'in). Kusali jamaa si Sunna wala faradhi kifaya, ambayo ikifanywa na baadhi ya Waislamu inatosheleza.

Kama ingelikuwa ni Sunna, basi wale walio katika mazingira ya vita wangepewa msamaha; na kama hukumu yake ingekuwa ni faradhi kifaya, basi kundi la pili lingefutiwa madhambi kwa sababu kundi la kwanza lilikwishatekeleza ibada ya sala kwa niaba ya kundi la pili. Ufafanuzi huu unaonesha wazi ulazima wa sala ya jamaa.

Malik bin Al–Huwairith (Allah amridhie) amesema kuwa, aliishi kwa Mtume pamoja na kundi lake (wenzake) kwa muda wa siku 20, Mtume akawaambia: "Rudini katika familia zenu mkawafundishe kusali, na sala inapowadia mtu mmoja aadhini, na mumteue mkubwa wenu awe Imam."

Huu ni ushahidi kuwa sala ya jamaa ni wajibu unaomhusu kila Muislamu mwanaume. Hata wenye ulemavu hawakuruhusiwa kuacha sala ya jamaa bila sababu za msingi. Abu Huraira (Allah amridhie) amesimulia kuwa, mtu mmoja mwenye ulemavu wa macho alimjia Mtume wa Allah (rehema na amani zimshukie) akamuomba ruhusa ya kusali nyumbani kwake kwa kuwa hana mtu wa kumsaidia kufika msikitini.

Mtume alimruhusu kusali nyumbani lakini kabla hajaondoka alimwiita na kumuuliza: "Je, unaisikia adhana (wito wa sala)." Yule mtu akamjibu: "Ndiyo." Mtume akamwambia: "Hudhuria sala ya jamaa msikitini." Kwa hiyo, sala ya jamaa ni faradhi ya lazima kwa kila Muislamu mwanaume aliye na uwezo wa kuitekeleza; na anayeacha kuitekeleza kwa makusudi atapata madhambi yanayohusisha adhabu na hatari ya kufeli katika ibada zote.

**TUJIFUNZE**
**AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)**

Na Junaynat Ally Dama




# Mambo 7 AI haiwezi kuchukua nafasi ya mwanadamu

Katika mijadala mingi ya sasa kuhusu akili bandia (AI), hofu moja imekuwa ikijirudia: mashine zitachukua kazi za binadamu. Lakini uchunguzi wa karibu unaonyesha picha tofauti kidogo.

Kadiri teknolojia inavyozidi kuwa na nguvu, ndivyo baadhi ya uwezo wa kibinadamu unavyokuwa na thamani zaidi. Historia ya maendeleo ya teknolojia inaonyesha jambo hili mara kwa mara.

Katika karne ya 19, zaidi ya asilimia 90 ya Wamarekani walifanya kazi katika kilimo. Leo ni chini ya asilimia mbili. Hata hivyo, watu hawakupotea; walibadilika kuwa wahandisi, walimu, wabunifu na wafanyabiashara. Mashine ya kufua haikuondoa kazi tu, bali ilibadilisha muundo wa jamii. Vivyo hivyo, AI inaondoa kazi za kawaida za kiakili, lakini inafungua nafasi kwa kile kinachoweza kuitwa "kazi ya ubinadamu".

Hapa ndipo zinapojitokeza stadi saba muhimu ambazo mashine zinaweza kusaidia, lakini haziwezi kuzimiliki kikamilifu.

Kwanza: hekima na uchambuzi wa kina. AI inaweza kuchakata taarifa nyingi kwa sekunde chache, lakini haiwezi kuelewa kikamilifu athari za maamuzi katika maisha halisi.

Binadamu bado ana jukumu la kuamua si tu nini kinawezekana kufanywa, bali nini kinapaswa kufanywa. Ndiyo sababu viongozi wakubwa hulipwa si kwa sababu wanajua taarifa nyingi, bali kwa sababu wana uwezo wa kufanya maamuzi sahihi katika mazingira yasiyo na uhakika.

### Maono na kusudi.

Mashine zinaweza kusaidia kufikia malengo yaliyowekwa, lakini haziwezi kuunda ndoto yenye maana. Historia inaonyesha kwamba mabadiliko makubwa katika jamii yamechochewa na watu walioweza kuona dunia tofauti na ilivyo sasa. Maono hayo ndiyo yanayovutia wengine kujiunga na safari.

Tatu: uhusiano wa kweli wa kibinadamu.

Katika dunia inayozidi kuwa ya kidijitali, uwezo wa kuzungumza kwa dhati na mtu mwingine unakuwa rasilimali adimu. AI inaweza kuiga huruma, lakini haiwezi kuhisi.n Walimu bora, viongozi bora na hata wanahabari bora hutegemea uwezo huu wa kuelewa hisia na hali ya watu wengine.

Nne: ustawi wa ndani na kujitambua. Kasi ya teknolojia inazidi kuongezeka, lakini akili ya binadamu bado inahitaji muda wa kutafakari. Uwezo wa kuwa mtulivu, kujitambua na kufanya kazi kwa utulivu wa ndani ni silaha muhimu katika ulimwengu wenye kelele nyingi za taarifa.

### Ladha na uamuzi wa kimaadili au kisanii.

AI inaweza kuchambua mifumo katika sanaa, muziki au maandishi, lakini haiwezi kuelewa kwa kina uzuri au maana yake katika maisha ya binadamu. Uamuzi kuhusu nini kina thamani au kinagusa hisia za watu bado unategemea uzoefu wa kibinadamu.

### Hisia za ndani au intuition.

Mara nyingi watu wenye uzoefu mkubwa hutambua fursa au hatari kabla hata data haijaonyesha wazi. Intuition hii hutokana na miaka ya maisha, makosa, mafanikio na uchunguzi wa mazingira. Hiki ni kitu ambacho algoritimu zinaweza kukaribia, lakini si kuishi nacho.

### Saba: akili ya kihisia (emotional intelligence).


Mahusiano ya kikazi, uongozi na hata biashara hutegemea uwezo wa kusoma hali za watu, kuelewa hisia zisizosemwa na kujenga uami-

رمضان

MAKALA MAALUM

0712 690 811

NA SHEIKH SEIF RUGA



# Fahamu mambo yanayoharibu swaumu

**Yanayobatilisha funga ya Ramadhan ni yale yanayoitengua na kuondosha uhalisia wa funga na kujizuilia. Mambo haya ndiyo yanayoitwa kwa lugha nyingine 'Vitenguzi vya swaumu'. Mambo yanayofunguza swaumu yapo aina nyingi. Kuna ambayo wanazuoni wamekubaliana kwa pamoja kuwa yanafunguza, na kuna yale waliyotofautiana.**

**Pia katika mambo hayo, kuna yanayowajibisha kulipa tu, na yale yanayowajibisha kulipa na kutoa kafara. Kisha, kuna yanayobatilisha funga kwa kuingiza kitu ndani ya tumbo la aliyefunga, na mengine ni kwa kutoka damu ya hedhi au nifasi, na kwa njia ya kujamiiana. Vilevile, yapo yanayopatikana kwa njia nyingine kama kujitapisha kwa makusudi. Ufuatao ni mchanganuo wa mambo yanayofunguza swaumu:**

## Kujamiiana mchana wa Ramadhan

Jopo la wanazuoni wote wa umma wa Kiislamu wamekubaliana kwamba, mtu aliyemuingilia mkewe, au mke na mume watakapofanya tendo la ndoa mchana wa mwezi wa Ramadhan kwa makusudi, swaumu yao itakuwa imeharibika na watapaswa kutubu na kumuomba Allah msamaha sambamba na kuilipa siku hiyo waliyojamiiana.

Pia, kila mmoja kati yao ni lazima atoe kafara kwa kumwacha huru mtumwa. Ikiwa hakuna mtumwa atafunga miezi miwili mfululizo baada ya kumalizika mwezi wa Ramadhan. Hairuhusiwi kukatisha swaumu isipokuwa kwa udhuru wa kisharia, kama kupatwa na hedhi au nifasi kwa mwanamke, au katika siku ya Idd au siku za tashriq (mwezi 11, 12 na 13 Dhul–Hijja).

Atakayekatisha kufunga bila udhuru japo kwa siku moja, atalazimika kuanza upya ili kukamilisha mfululizo uliotajwa. Na iwapo kufunga miezi miwili itashindikana atawalisha masikini 60, kwa kutoa kiasi cha robo pishi (takribani gramu 562 au nusu na robo) ya chakula pendwa au chakula cha kawaida kinachotumiwa na watu wa nchi yake.

Na hairuhusiwi kulisha masikini isipokuwa kama hawezi kufunga kwa udhuru unaoruhusiwa, mfano ugonjwa au hofu ya kupata madhara.

## Kutoa manii (mbegu za uzazi) kwa kukusudia

Iwapo aliyefunga atatoa manii kwa njia ya kumbusu mkewe, kumgusa, kujichua (masturbation), au kwa njia nyingine yoyote, swaumu yake itabatilika na atawajibika kuilipa siku hiyo.

Na kama atambusu au kumgusa pasina kutokwa na manii, swaumu yake ni sahihi na hatoi fidia yoyote. Ama aliyetokwa na manii akiwa usingizini katika mchana wa Ramadhan, au aliyetokwa na manii kutokana na kuwaza tu bila tendo la kimwili, swaumu yake ni sahihi.

## Kula au kunywa

Mtu aliyefunga akiingiza kitu kwa njia ya kula au kunywa, kikafika hadi ndani ya tumbo lake kwa makusudi hali ya kuwa amefunga, atakuwa amefungua.

Vilevile, swaumu inabatilika kwa kuingiza kitu hadi ndani ya tumbo kwa makusudi kwa njia isiyokuwa ya kula au kunywa, ikiwamo kwa mfano, kupitia njia ya puani na kufika hadi ndani ya tumbo, au mtu kuwekewa sindano za lishe (drips) zinazochukua nafasi ya chakula na kinywaji, au kuongezewa damu kwa njia ya sindano kiasi cha kumpa nguvu.

Ama sindano zisizo za lishe haziharibu swaumu, maadamu hazifiki tumboni kama ilivyotajwa. Na wala swaumu haibatiliki kwa kuingia vumbi au moshi kupitia puani, au kwa kitendo cha kumeza nzi, yaani vitu ambavyo huna uwezo wa kujikinga navyo.


## Kupiga chuku na kujitapisha

Kupiga chuku (hijama) ni kile kitendo cha kukata sehemu ya juu ya ngozi kwa makusudi ili kutoa damu mwilini, bila kukata mishipa mikubwa. Mtume wa Allah (rehema na amani zimshukie) amesema: "Kupiga chuku kunamfunguza mpigwa chuku na mpiga chuku." [Tirmidhi].

Hivyo, hairuhusiwi aliyefunga swaumu ya wajibu kutoa damu yake kwa hiari – iwe kwa kupiga chuku au kumchangia damu mgonjwa, isipokuwa katika hali ya dharura kubwa kwa sharti asidhurike, na atakula siku hiyo kisha atailipa baada ya Ramadhan kumalizika.

Swaumu ya mtu haibatiliki kwa damu itokayo puani, damu ya ugonjwa (isiyokuwa ya hedhi), damu ya jeraha, na ile itokayo kwenye fizi baada ya kung'olewa jino au kujing'ata, kwa sharti tu asiimeze damu hiyo.

Aidha, atakapotapika aliyefunga kwa bahati mbaya bila ya ridhaa yake, swaumu yake itakuwa sahihi. Imekuja hadith kutoka kwa Mtume (rehema na amani ya Allah ziwe juu yake) akisema: "Mtu aliyeshindwa na matapishi hatailipa siku hiyo, na yule atakayejitapisha kwa makusudi ailipe." Ama kujitapisha kwa makusudi kunabatilisha swaumu, kwa ushahidi wa hadith tuliyoitaja.



**MAKALA YA AFYA**
**0764 101 018**



**DKT.**
**Omar A. Kasuwi**
**Daktari Bingwa Mshauri wa magonjwa Moyo!**
**Hospitali ya Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA)**

# Shinikizo la juu la damu: Muuaji wa kimyakimya na chanzo cha moyo kushindwa kufanya kazi

Takwimu zinatisha! - Mtu mmoja kati ya watatu duniani ana Shinikizo la Juu la Damu (HT), 50% ya wenye tatizo hili hawafahamu kuwa wana tatizo hilo. Pia, shinikizo la juu la Systolic husababisha kifo cha mmoja kati ya watu 5 wenye shinikizo la damu.

## Pengo katika udhibiti (control gap)

Takwimu zinazidi kuonesha kuwa, wagonjwa wanne kati ya watano hawajadhibitiwa vizuri shinikizo lao la damu ikimaanisha shinikizo lao la damu bado ziko juu; na mgonjwa mmoja kati ya wawili hafuati maelekezo ya dawa ipasavyo.

Si hayo tu, tafiti zinaonyesha kuwa asilimia 86.3 ya wagonjwa wote wa shinikizo la damu wapo kwenye hatari kubwa sana, lakini madaktari wengi kwa mazoea huchukulia kuwa ni kiwango cha wastani au si hatari kabisa.

Tahadhari muhimu ya kuzingatia hapa ni kuwa, hali hii husababisha wagonjwa kupewa matibabu ya kiwango cha chini kuliko mahitaji yao halisi au inavyostahili.

## Dawa

Miongozo ya kimataifa sasa inashauri matumizi ya kidonge kimoja mseto (SPC) chenye dawa mbili au tatu ndani yake kwani hurahisisha utumiaji, huongeza ufuatiliaji wa dawa, na hudhibiti shinikizo la damu kwa uhakika zaidi. Dawa hizi mara nyingi huuzwa kwa bei ya juu, lakini kwa hakika huo ni uwekezaji bora kwa usalama wa maisha yako.

Muhimu zaidi hapa ni kuhakikisha kila mwana nchi anafahamu hatari ya kuwa na shinikizo la damu na hivyo afuate ushauri wa madaktari vizuri. Mambo matatu ni muhimu:

Kwanza, pima shindikizo la damu (BP) asubuhi mara baada ya kuamka na jioni kabla ya kulala ama kwa ushauri wa daktari wako.

Pili, chunguza na fuatilia zaidi maradhi haya: kisukari, uzito wa ziada na historia ya familia. Tatu, lenga kuwa katika viwango salama vya BP ambavyo ni – < 120/85 mmHg kwa wengi; na <130/80 mmHg kwa walio na maradhi kama kisukari, na magonjwa ya moyo .

## Fuata utaratibu wa kuishi kiafya

Ili kuishi kiafya, punguza vyakula vyenye chumvi hatarishi, hasa kwa ulaji tuliouzoea sana wa nyama choma, kuku choma, kuku wa ndoo, kisahani nk. Vyakula hivi maandalizi yake si salama. Kadhalika, kula mboga, matunda, korosho na samaki.

Vilevile, fanya mazoezi dakika 45 kwa siku kila siku, ama mara tatu kwa wiki. Lakini pia acha kutumia tumbaku, kunywa pombe, na kutumia madawa ya kuleya . Kadhalika, dhibiti uzito, na msongo wa mawazo

## Tujifuze kutumia dawa kwa usahihi


Usikatishe ama kuacha dawa bila ushauri wa daktari wako, lakini pia tafuta ushauri wa pili pia pale inapobidi, usiridhike kirahisi. Kumbuka ni kuhusu usalama wa maisha yako si ya daktari. Angalia hatari ya jumla: Omba daktari wako akufanyie uchunguzi mara kwa mara (risk assessment) ili kuangalia na kung'amua uwezekano wa mabadiliko katika siku zijazo katika moyo, figo, na ubongo. Tafuta msaada wa haraka endapo shinikizo la damu liko – BP ni zaidi ya 180/100 mmgh ama pia ikiambana maumivu ya kifua, kizunguzungu kikali, kupooza upande mmoja, au upungufu wa hewa.

## Ushauri wa kutumia kifaa cha upimaji -Home BP monitor!

Kwa ufuatiliaji wa shinikizo la damu nyumbani, inashauriwa zaidi kuwa na kifaa hiki cha uchunguzi nyumbani. Kifaa aina hii ya Omron M4 Intelli IT kinapendekezwa zaidi kwa sababum; kwanza, kina 'smart cuff' inayopunguza makosa ya upimaji kuliko aina nyingine zilizoko katika soko.

Sababu ya pili, Omron M4 Intelli IT, kinahifadhi matokeo na inaweza kuunganishwa na simu kupitia App kwa ajili ya kumbukumbu yako lakini kwa ajili ya kumuonesha daktari wako unapoenda kliniki.

Sababu ya tatu, kifaa hiki kimetambulika na mashirika ya kimataifa ya kiafya; na nne hiki ni kifaa rahisi kutumia kwa wagonjwa wa muda mrefu na wazee. Tano na mwisho, kifaa hiki kinawezesha utambuzi wa haraka wa mwenendo mbaya wa moyo wako hatarishi kwa kupata kiharusi (AF rhythm detection).



NA JUNAYNAT ALLY DAMA

# Matumizi ya bangi yahusisishwa na matatizo ya afya ya akili

Utafiti mpya nchini Canada umebainisha uhusiano chanya kati ya matumizi ya bangi na afya ya akili. Watafiti kutoka Chuo Kikuu cha McMaster wamebaini kuwa watu wanaotumia bangi wana uwezekano mkubwa zaidi wa kuripoti matatizo kama wasiwasi, msongo wa mawazo, unyogovu na mawazo ya kujiua.

Utafiti huo, uliochapishwa Februari 2026 katika jarida la The Canadian Journal of Psychiatry, ulihusisha uchambuzi wa takwimu za zaidi ya watu 35,000. Data hizo zilitokana na tafiti za kitaifa zilizofanywa kati ya mwaka 2012 na 2022. Matokeo yalionyesha kuwa matumizi ya bangi yaliongezeka katika kipindi hicho, huku idadi ya watu wanaoripoti matatizo ya afya ya akili nayo ikiongezeka.

Ingawa utafiti haujaonyesha moja kwa moja kwamba bangi ndiyo chanzo cha matatizo hayo, mambo hayo mawili yanaonekana kuenda pamoja. Ongezeko kubwa la mawazo ya kujiua lilionekana kwa vijana Wataalamu wanahimiza elimu kwa umma na uchunguzi wa mapema wa afya ya akili kwa watumiaji wa bangi.



# Siwezi kukushinda kwa jambo lolote milele

**Zaid bin Aslam amepokea hadith kutoka kwa baba yake kuwa, siku moja alimsikia Umar bin Khattwab (Allah amridhie) akisema: "Mtume wa Allah (rehema.na amani zimshukie) alituamuru tutoe sadaka katika wakati ambao nilikuwa na mali, nikasema, 'Leo nitahakikisha namshinda Abubakar kama itatokea (itawezekana) kumshinda, nikaja na nusu ya mali yangu."' Mtume (rehema na amani zimshukie) akaniuliza: "Umebakiza nini kwa ajili ya familia yako?" Nikajibu: "Nimebakiza mfano wa hiyo niliyotoa (nusu iliyobaki)." Kisha Abubakar akaja na mali yake yote, Mtume (rehema na amani zimshukie) akamuuliza: "Umebakiza nini kwa ajili yao?" Akasema: "(Familia yangu) nimewaachia Allah na Mtume wake (yaani hakubakiza kitu)." Umar akasema: "Sitaweza kukushinda kwa jambo lolote milele."**

## Mafundisho ya tukio hili:

Tukio hili linaonesha pupa waliyokuwa nayo wema waliotangulia katika suala la kujitolea mali zao katika milango ya kheri. Ilikuwa kawaida kujitolea sehemu ya mali yao kwa ajili ya Allah Mtukufu na kutekeleza lengo la uwepo wao duniani.

Aghlabu Mtume (rehema na amani zimshukie) alipowahamasisha Masahaba kujitolea kwa ajili ya kuipambania dini ya Allah, hawakusita hata kidogo kuitikia wito huo. Kila mmoja alidhamiria kumshinda mwenzake na kumtangulia katika kheri hiyo.

Hivi sasa tuko ndani ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan, mwezi wa kujipinda na kujitoa kwa dhati katika kila aina ya kheri iliyopo mbele yetu. Pamoja na wingi wa mambo ya kheri ambayo ni fursa kwa kila Muislamu kujibidiisha kuyafanya, kuna mambo ambayo msingi wake ni kujitolea mali katika njia ya Allah kwa ajili ya kujikurubisha kwake ndani ya siku bora za mwezi huu wa Ramadhan.

## Kutoa sadaka

Kutoa sadaka ni ibada bora inayomkurubisha mja kwa Allah Ta'ala hasa ndani ya mwezi wa Ramadhan. Katika nukuu mbalimbali za Sunna, tunajifunza namna Mtume (rehema na amani zimahukie) alivyokuwa mstari wa mbele katika kuwasaidia watu. Masahaba (Allah awaridhie), nao hawakubaki nyuma katika kuiga mwenendo huu wa Mtume.

Tunaelezwa kuwa, mjumbe wa Allah (rehema na amani zimshukie) alikuwa mkarimu kuliko watu wote, na alikuwa mkarimu zaidi katika mwezi wa Ramadhan. Ukarimu wake katika kufanya mambo ya kheri ulikuwa kama upepo unaovuma kwa kasi. Mtume amesema: "Sadaka iliyo bora zaidi ni ile inayotolewa katika (mwezi wa) Ramadhan." [Tirmidhi kutoka kwa Anas].

Hadith nyingine kutoka kwa Talha bin Yahya inaeleza kwamba, bibi yake aitwae Su'da bint Awf (mke wa Talha bin Ubaydillah) alisema: "Siku moja Talha aliingia kwangu akiwa na huzuni, nikamuuliza: 'Mbona naona uso wako umebadilika? Je, kuna jambo nimekufanyia?'"

Akasema: "Hapana, wewe ni mke mwema." Nikamuuliza: "Kuna nini basi?" Akasema: "Mali niliyonayo imekuwa nyingi na imeniletea mzigo moyoni." Nikamwambia: "Basi igawanye." Akaigawa mali hiyo kiasi ambacho haikubaki hata dirhamu moja, ingawa kabla ya hapo alikuwa na dirhamu 400,000.

Naam! Hivi ndivyo Mtume na Masahaba wake walivyotuachia alama na athari njema ya namna Muislamu anavyotakiwa ajitolee mali yake katika njia ya Allah. Sadaka katika mwezi wa Ramadhan ina fadhila ya kipekee.

Unaweza kutoa sadaka ndani ya mwezi wa Ramadhan kadri ya uwezo wako kwa sura nyingi, ikiwamo kulisha watu chakula. Allah Mtukufu anasema: "Na wanawalisha chakula pamoja na kukipenda, masikini, yatima na mateka. (Wanasema): Hakika sisi tunakulisheni kwa ajili ya Allah tu, hatutaki kwenu malipo wala shukrani. Hakika sisi tunamuogopa Mola wetu kwa siku yenye shida na taabu. Basi Allah akawalinda na shari ya siku hiyo, akawakutanisha na nuru na furaha, na akawalipa kwa uvumilivu wao Pepo na hariri." [Qur'an, 76:8–12].

Wema waliopita walikuwa wanahimiza sana kulisha watu chakula, na waliitanguliza huduma hii juu ya ibada nyingi. Haishurutishwi umlishe fukara tu, hata kumlisha ndugu mwema ni kheri pia. Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Enyi watu! Toeni salamu, lisheni chakula, dumisheni undugu, na swalini usiku watu wakiwa wamelala, mtaingia Peponi kwa amani." [Ahmad na Tirmidhi].

Miongoni mwa watu waliopendelea sana kulisha watu chakula ni Abdullah bin Umar (Allah amridhie). Sahaba huyu Mtukufu alikuwa anafungua swaumu (anakula futari) pamoja na mayatima na masikini. Kadhalika, Masahaba wengine wengi walikuwa wanawalisha na kuwahudumia wenzao. Kulisha watu chakula hupandikiza mapenzi baina ya ndugu na ni sababu ya kuingia Peponi. Pia hutoa fursa ya kukaa na watu wema na kupitia chakula hicho hupata nguvu ya kufanya ibada.

Jambo hili linaunga na kutia nguvu undugu, ujirani na ujamaa, kwani kupitia mwaliko wa chakula wanakutana masikini na matajiri, marafiki, na hata wale wasiojuana hutokea kufahamiana katika matukio ya namna hii. Kulisha chakula ni takrima inayopendwa na watu wengi kutokana umuhimu wake katika kujenga upendo na ujamaa, ambao ni vigumu kuujenga kwa njia nyingine. Ikiwa mtu hawezi kulifanya hilo kwa kiwango cha kuwakusanya watu wengi, basi afanye hivyo hata kwa mtu mmoja au wawili, kwani Allah humlipa mtu kwa nia yake na uthubutu wake wa kufanya hivyo kwa ajili ya kutaka radhi zake.

## Kufuturisha waliofunga


Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Atakayemfuturisha aliyefunga anapata malipo (thawabu) mfano wa malipo ya aliyemfuturisha, na hakipungui chochote katika malipo ya mfungaji." [Ahmad na Nasai].

Kuna njia nyingi za kuwafuturisha watu; unaweza kuandaa chakula cha futari na kuwakaribisha watu waje kula, au kuandaa kitu chochote ambacho unahisi kuwa ni bora kwa mfungaji na ni rahisi kukitumia kwa ajili ya kufungua kinywa, mfano tende, maji au matunda mengine ambayo ni mwafaka.

Si lazima kuandaa chakula kingi na kuwaalika watu ili kupata fadhila za kufuturisha, hapana! Fadhila hizi utazipata kwa kujipanga vizuri kwa kuhakikisha kuwa unaandaa chochote ambacho ni rahisi kutumika kwa ajili ya kufungua kinywa.

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Njia tano wazazi wanafundisha watoto tabia ya uongo bila kujijua



**Wazazi wengi wana lengo moja la msingi katika malezi: kuwalea watoto wanaosema ukweli, wanaowajibika, na wanaoishi kwa uadilifu. Lakini kwa namna ya kushangaza, mazingira ya nyumbani yanaweza wakati mwingine kufundisha somo tofauti kabisa.**

**Wakati mtoto anapoona kwamba kusema ukweli kunaadhibiwa huku kusema uongo kunaweza kumuepusha na matatizo, akili yake huanza kuhusisha uongo na "usalama."**

**Kwa lugha rahisi, watoto hujifunza kwamba ukweli una gharama, lakini uongo una faida. Mara nyingi hali hii haisababishwi na makusudi ya wazazi; hutokea kupitia tabia ndogo ndogo za mawasiliano.**

**Hapa chini kuna makosa matano ya kawaida ambayo yanaweza kufanya watoto waone kusema uongo ni njia rahisi zaidi.**

## *Mosi,* kuuliza swali ambalo mzazi anajua jibu lake

Mfano wa kawaida ni mzazi kumuuliza mtoto: "Je, ulimpiga ndugu yako?" ilhali mzazi tayari aliona tukio hilo. Swali hili linaweka mtoto katika mtego wa kisaikolojia: akisema ukweli ataingia matatani, lakini akisema uongo anaweza kujaribu kujiokoa.

Kwa mtoto, hili linakuwa chaguo la haraka kati ya ukweli na adhabu. Badala yake, wataalamu wa malezi wanashauri mzazi kueleza alichokiona moja kwa moja: "Nimeona umempiga ndugu yako. Hebu tuzungumze kilichotokea." Njia hii inaondoa mtego wa uongo na inaelekeza mazungumzo kwenye kutatua tatizo.

## *Pili,* kuonyesha hasira kubwa kwa makosa madogo

Fikiria mtoto anapokuja kukiri kwamba alivunja kitu kwa bahati mbaya, halafu mzazi analipuka kwa hasira: "Ulikuwa wapi akili yako? Si nilikwambia uwe makini?"

Utafiti wa saikolojia ya malezi unaonyesha kuwa mazingira ya hofu yanawafanya watoto wajifunze kuficha makosa. Wanahusisha ukweli na adhabu, hivyo mara nyingine huchagua kimya au uongo ili kujilinda.

Njia bora zaidi ni kuthamini uaminifu kwanza: "Asante kwa kuniambia ukweli. Ajali hutokea. Hebu tuone namna ya kurekebisha." Hii inafundisha mtoto kuwa kusema ukweli ni hatua ya kwanza ya kutatua tatizo.

## *Tatu,* kutothamini ukweli unaposemwa

Watoto pia huangalia kama kusema ukweli kunaleta tofauti yoyote. Ikiwa mtoto anakiri kosa na bado anapewa adhabu ile ile kama angekamatwa katika uongo, ujumbe unaofikishwa ni wazi: kusema ukweli hakusaidii.

Kwa sababu hiyo, wataalamu wanashauri wazazi kutambua ujasiri wa kusema ukweli. Mzazi anaweza kusema: "Nashukuru umeniambia ukweli. Hiyo inahitaji ujasiri." Mara nyingi hata kupunguza au kurekebisha adhabu kunaweza kufundisha kwamba uaminifu una thamani.

## *Nne,* kutarajia ukamilifu

Wazazi wengine huwasisitiza watoto kuwa hawapaswi kufanya makosa kabisa, kwa kauli kama: "Nimevunjika moyo sana na wewe," au "Nilitarajia zaidi kutoka kwako."

Kauli hizi zinaweza kumfanya mtoto ahisi kwamba kosa ni sawa na kushindwa kama mtu. Wakati makosa yanapoonekana kama aibu kubwa, watoto hujifunza kuyaficha badala ya kuyarekebisha.

Njia yenye afya zaidi ni kuwafundisha watoto kwamba makosa ni sehemu ya kujifunza: "Kila mtu hukosea. Muhimu ni tunajifunza nini baada ya hapo."

## *Tano,* kutokuwa mfano wa uaminifu

Watoto hujifunza zaidi kwa kuangalia kuliko kusikiliza. Mzazi anapomwambia mtoto: "Mwambie mtu huyo sipo nyumbani," au kutoa visingizio visivyo vya kweli, mtoto anapata somo lisilo la moja kwa moja kwamba uongo unaweza kutumika kama chombo cha urahisi.

Kwa maneno mengine, watoto huiga tabia wanazoziona. Ikiwa wazazi wanataka uaminifu, lazima nao wawe mfano wa uaminifu.

## Somo kubwa la malezi

Kiini cha suala hili ni mazingira ya mawasiliano nyumbani. Watoto wanapohisi kwamba kusema ukweli kunasababisha mazungumzo, msaada na suluhisho, wanakuwa na uwezekano mkubwa wa kusema ukweli. Lakini wanapohisi kwamba ukweli unaleta aibu, hasira au adhabu kali, wanaanza kutafuta njia ya kujilinda.

Kwa hiyo, kuwafundisha watoto uaminifu si suala la kuwaambia wasiseme uongo pekee. Ni suala la kujenga mazingira ambapo ukweli ni salama, unathaminiwa, na unasaidia kutatua matatizo. Ndipo watoto hujifunza kwamba uaminifu si tu maadili mazuri – bali pia ni njia bora ya kuishi.

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494

SEHEMU YA 3



# VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

# SIMULIZI YA AKINA THAMOUD WATU WA NABII SWALEH

**Katika makala iliyopita tuliona akina thamoud walivyopinga mafunzo na ujumbe aliokuja nao Mtume wao. Wakuu walionesha msimamo wao kwamba wao ndio wa kwanza kuyakufuru mafunzo na wakawazuia wengine waliotaka kuujua na kuufuata ukweli.**

## Muujiza wa Ngamia

Watu wa Mtume Swaleh (amani ya Allah imshukie) katika kuonesha upinzani wao mbele ya Mtume wao walimwambia kuwa kama yeye kweli ni Mtume wa Allah, basi amuombe Mola wake awatolee ngamia kwenye jabali. Walimwambia kamwe hawatomuamini mpaka awaoneshe muujiza huo, wakiamini kwamba atashindwa tu.

Kama ilivyokuwa kwa Mitume wengine, Mtume Swaleh alikuwa na Imani na tawakuli (kumtegemea Allah) kwa hali ya juu kabisa. Aliamini kwamba, Allah ni Muweza wa kila kitu.

Basi Mtume Swaleh (amani ya Allah imshukie) akamuomba Mola wake kwa unyenyekevu mkubwa. Naam, ngamia jike mwenye mimba akatoka kwenye jabali kavu watu wakamshuhudia, Allaahu Akbar!

Hata hivyo, wapinzani hao pamoja na kushangazwa sana na tukio hilo, hawakuamini, na wakabaki katika kufuru yao.

## Wasifu wa ngamia

Ngamia alikuwa mkubwa na wa ajabu sana. Alikuwa na uwezo mkubwa wa kula na kunywa. Qur'an inasimulia: "Wakasema, 'Hakika wewe ni miongoni mwa waliorogwa (wakakosa hekima), wewe si chochote ila ni mtu kama sisi, basi lete muujiza ikiwa ni miongoni mwa wasemao kweli.' Akasema, 'Huyu ngamia jike, lakini awe na zamu yake ya kunywa na nyinyi muwe na zamu yenu ya kuteka katika siku maalum, wala msimguse kwa ubaya isije ikakushikeni adhabu ya siku kubwa.'" [Qur'an, 26:153-156]

Na katika sura nyengine, Qur'an inasema: "Na enyi watu wangu, huyu ngamia wa Allah, ni ishara kwenu (mliyoitaka kwangu) basi muacheni ale katika ardhi ya Mwenyezi Mungu wala msimguse kwa ubaya wowote, isije ikakuangamizeni adhabu iliyokaribu." [Qur'an, 11:64].

Kina Thamoud walitekeleza agizo hilo kwa shida sana. "Mtaka nyingi nasaba humkuta mingi misiba", ngamia aliyewafikia katika mji wao sasa ikawa kero kwao. Ilipofika zamu yake, alimaliza maji ya mji mzima, hadi mifugo yao inakosa maji.

Isitoshe, mifugo hiyo ilimuogopa ngamia wa ajabu kiasi cha kukimbia kila walipomuona. Ngamia akawa gumzo pekee la watu katika makazi yao; masokoni, majumbani, njiani na katika barza zao.

Mtume Swaleh (amani ya Allah imshukie) akiishuhudia hali hiyo, alizidi kuwatahadharisha watu wake wasije kumuua ngamia wa muujiza walimtaka wenyewe. Alijua kwamba, kitendo hicho kitakuwa sababu ya kuwafika adhabu isiyo kifani.

## Thamuod wapanga mkakati wa kumuua ngamia

Thamuod waliitisha kikao mkakati kilichopanga mauaji. Waliulizana: "Nani atamuua ngamia?" Akasema mmoja wao: "Mimi niko tayari kumuua." Mwengine naye akasema: "Na mimi niko tayari kumuua." Qur'an imemtaja kwa "Ashqaahaa" (muovu kuliko wote).

Watu wawili hao walimsubiri, alipotoka tu mmoja akampiga mshale na wa pili akamchinja.

## Yaliyojiri baada ya Thamoud kumuua ngamia

Mtume Swaleh (amani ya Allah imshukie) aliposikia kwamba ngamia ameuliwa alisikitika na aliogopa sana.

Baada ya kumuua ngamia, waliachiwa waendelee na vipumbazanafsi vyao kwa siku tatu, huku wakipongezana kwa ushujaa walioufanya, wakiamini kwamba, wamemshinda Swaleh na hakuna adhabu yoyote itakayowafika kama alivyowaahidi.

Baada ya siku tatu kupita, adhabu iliwafika. Ulikuwa ni ukulele tu uliopigwa na Malaika, ukasababisha tetemeko kubwa la ardhi katika makazi yao, mara wakazima (wakafa) na mji wao kuzizima, mashamba, visima, makasri yao yakabaki matupu, kama hawakuwahi kuishi humo binadamu!

Qur'an inasimulia: "Wakamchinja, basi (Swaleh) akasema, 'Stareheni katika mji wenu (huu) siku tatu (tu kisha mtaadhibiwa) hiyo ni ahadi isiyo ya uongo. Basi ilipofika amri yetu tulimuokoa Swaleh na walioamini pamoja naye kwa rehema Yetu katika khizaa ya siku hiyo. Hakika, Mola wako ndiye Mwenye nguvu, Mwenye kushinda. Na wale waliodhulumu (nafsi zao) uliwaangamiza ukulele wakapambaukiwa wametulia (tuli) (wamekufa) katika majumba yao. Kama kwamba hawakuwemo humo. Sikilzeni, hakika Thamoud walimkufuru Mola wao, basi Thamoud wamepotelea mbali" [Qur'an, 11:65-68].

Tusome tena aya ifuatayo: "Wakamtumbua (wakamuua) ngamia na wakaasi amri ya Mola wao na wakasema, 'Ewe Saleh tuletee unayotuahidi ikiwa wewe ni miongoni mwa mitume.' Mtetemeko wa ardhi ukawanyakua na wakawa wamekufa humo katika miji yao." [Qur'an, 7:77-78].

UKHTI FATIMA SS

# Siri saba za kujenga haiba na mvuto kwa watu

**Katika maisha ya kila siku, watu wengi huamini kuwa mvuto wa kijamii—au kile kinachoitwa charisma—ni kipaji cha kuzaliwa nacho. Wengine huonekana kuvutia watu kwa urahisi: wanapoingia chumbani watu wanawasikiliza, wanapozungumza wengine wanajisikia huru na wanapenda kuwa karibu nao. Lakini wanasaikolojia na wataalamu wa mawasiliano wanasema jambo tofauti. Kwa kiasi kikubwa, charisma ni ujuzi unaoweza kujifunzwa.**

**Mmoja wa watu walioandika sana kuhusu sanaa ya kuwasiliana na kuvutia watu ni Dale Carnegie, mwandishi wa kitabu maarufu How to Win Friends and Influence People. Katika mafundisho yake kuhusu mahusiano ya kijamii, anataja kanuni kadhaa rahisi zinazoweza kumfanya mtu awe na mvuto mkubwa kwa wengine. Zifuatazo ni baadhi ya kanuni hizo saba.**

## Mosi, tabasamu ni mwanzo wa mvuto

Tabasamu ni lugha ya kimya ambayo karibu kila mtu anaielewa. Watafiti wa mawasiliano ya kijamii wanaonyesha kuwa tabasamu linaweza kuvunja ukuta wa kutoaminiana kati ya watu wawili ndani ya sekunde chache.

Unapokutana na mtu kwa mara ya kwanza, tabasamu nyepesi linaweza kumfanya ajisikie huru na kukaribishwa. Wakati wa mazungumzo, tabasamu pia husaidia kuonyesha kuwa unasikiliza na unafurahia mazungumzo. Kwa kifupi, ni ishara ndogo yenye athari kubwa katika kujenga uhusiano.

## Pili, mfanye mtu ajisikie muhimu

Moja ya mahitaji makubwa ya kisaikolojia ya binadamu ni kutambuliwa na kuthaminiwa. Watu wanapohisi kuwa wanaonekana na kusikilizwa, wanajisikia vizuri zaidi kuwa karibu na mtu anayewapa hisia hiyo.

Njia rahisi ya kufanya hivyo ni kuonyesha umakini wa kweli. Angalia macho ya mtu unapozungumza naye, uliza maswali kuhusu kile anachosema, na onyesha kuwa unavutiwa na maoni yake. Watu wengi hawakumbuki sana maneno uliyosema, lakini wanakumbuka jinsi ulivyowafanya wajisikie.

## Tatu, kuwa msikilizaji mzuri

Watu wengi wanapozungumza na wengine husubiri tu nafasi yao ya kujibu. Lakini msikilizaji mzuri hufanya kitu tofauti: husikiliza ili kuelewa.

Hii ina maana ya kumruhusu mtu mwingine aeleze mawazo yake bila kukatizwa, kuuliza maswali ya ufafanuzi na kujibu kwa uaminifu kile kilichosemwa. Kusikiliza kwa makini kunamfanya mtu ahisi kuthaminiwa, na mara nyingi huwa msingi wa uhusiano wa karibu.

## Nne, kumbuka majina ya watu

Kwa mujibu wa Carnegie, jina la mtu ni sauti tamu zaidi kwa masikio yake. Kukumbuka na kutumia jina la mtu katika mazungumzo kunaonyesha kuwa unamheshimu na unamchukulia kwa umuhimu. Wataalamu wa mawasiliano wanashauri kutumia jina la mtu mara chache katika mazungumzo—labda mara mbili au tatu—bila kupitiliza. Hii huongeza hisia ya ukaribu na uhusiano wa kibinadamu.

## Tano, lugha ya mwili inaongea zaidi ya maneno

Utafiti mwingi wa mawasiliano unaonyesha kuwa sehemu kubwa ya ujumbe wetu hutumwa kupitia lugha ya mwili kuliko maneno yenyewe. Msimamo wa mwili, macho, mikono na hata namna tunavyokaa vinaweza kuonyesha kujiamini au kutokuwa na uhakika.

Kudumisha mawasiliano ya macho, kusimama kwa kujiamini na kutumia ishara za wazi za mikono kunaweza kumfanya mtu aonekane mwenye kujiamini na anayekaribisha mazungumzo.

## Sita, jifunze kusimama kidogo kabla ya kujibu

Watu wengi hujibu haraka sana wanapoulizwa swali. Lakini kusimama kwa sekunde moja au mbili kabla ya kujibu kunaweza kuwa na athari kubwa. Kwanza, inaonyesha kuwa unafikiria kwa makini. Pili, inaongeza uzito wa maneno yako.

Tabia hii pia husaidia kuzuia majibu ya haraka yanayoweza kuleta migogoro au kutokuelewana.

## Saba, tumia ucheshi kwa kiasi

Ucheshi mdogo unaweza kufanya mazungumzo yawe mepesi na ya kuvutia. Watu wanapocheka pamoja, hisia ya ukaribu huongezeka. Hata hivyo, wataalamu wanashauri ucheshi uwe wa kawaida na usilazimishwe.

Kauli ndogo ya kuchekesha au tabasamu la pamoja mara nyingi hutosha kuleta hali ya urafiki katika mazungumzo.

Siri ya charisma haiko katika kujaribu kuwavutia watu kwa nguvu. Badala yake, iko katika kuwafanya watu wajisikie vizuri wanapokuwa karibu nawe. Tabasamu, kusikiliza, kuonyesha heshima na kutumia mawasiliano mazuri ya mwili ni mbinu rahisi lakini zenye nguvu.

Kwa maneno mengine, mtu anayevutia watu zaidi si yule anayezungumza sana, bali yule anayewafanya wengine wajisikie kusikilizwa, kuthaminiwa na kuheshimiwa.

NA UKHTI FATIMA



# Uwekezaji bora zaidi ni kuwekeza ndani yako mwenyewe

**Katika dunia ya biashara na maendeleo binafsi, watu wengi hutumia muda mwingi kufikiria jinsi ya kuwekeza fedha—katika ardhi, biashara, hisa au miradi mbalimbali. Lakini baadhi ya wataalamu wa uchumi na biashara wanasema kuna uwekezaji mmoja ambao una faida kubwa kuliko yote: kuwekeza ndani yako mwenyewe.**

Mwekezaji maarufu Warren Buffett aliwahi kusema, "Uwekezaji bora zaidi unaoweza kufanya ni kuwekeza ndani yako mwenyewe." Kauli hii ina maana kwamba maendeleo ya akili, ujuzi na afya ya mtu vinaweza kuwa rasilimali kubwa zaidi katika maisha yake.

Unapowekeza ndani yako mwenyewe, unaongeza uwezo wako wa kufikiri, kufanya maamuzi bora na kutumia fursa zinazojitokeza katika maisha. Kwa kifupi, wewe mwenyewe unakuwa rasilimali yako muhimu zaidi.

Moja ya njia muhimu za kuwekeza ndani yako ni kujifunza bila kukoma. Dunia ya leo inabadilika kwa kasi sana. Teknolojia mpya, mbinu mpya za biashara na maarifa mapya yanaendelea kujitokeza kila siku. Watu wanaoendelea kusoma vitabu, kuhudhuria mafunzo au kujifunza kozi mbalimbali wana uwezekano mkubwa wa kuendana na mabadiliko hayo. Kujifunza kunapanua fikra na kuongeza uwezo wa kuona fursa ambazo wengine wanaweza wasizionee.

Hatua nyingine muhimu ni kukuza ujuzi mpya. Ujuzi wa kitaaluma, ujuzi wa mawasiliano, uongozi au ubunifu unaweza kuongeza thamani ya mtu katika soko la ajira au katika biashara.

Kadri mtu anavyoongeza ujuzi wake, ndivyo anavyoongeza uwezo wake wa kutatua matatizo na kuunda fursa mpya za kipato.

Afya ya mwili pia ni sehemu muhimu ya uwekezaji binafsi. Mwili wenye afya humwezesha mtu kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na kuwa na nguvu ya kufikia malengo yake. Lishe bora, mazoezi na mapumziko ya kutosha vina athari kubwa katika ubora wa maisha na uwezo wa kufanya kazi kwa tija.

Mbali na afya ya mwili, afya ya akili nayo ina nafasi kubwa. Maisha ya kisasa yanaweza kuleta msongo wa mawazo, shinikizo la kazi na changamoto za kijamii. Ndiyo maana wataalamu wa saikolojia wanashauri watu kufanya mazoezi ya kutuliza akili kama vile kutafakari, kuandika mawazo yao au kufanya shughuli zinazowasaidia kupata utulivu wa kihisia. Akili iliyo tulivu husaidia kufanya maamuzi sahihi na kudumisha mahusiano mazuri.

Mazingira yanayomzunguka mtu pia yanaweza kuathiri maendeleo yake. Watu wanaokuzunguka wanaweza kukuinua au kukuvuta chini. Ndiyo maana ni muhimu kujizunguka na watu wenye mtazamo chanya, wanaokuhamasisha na kukusaidia kukua. Mazingira mazuri mara nyingi huchochea nidhamu, motisha na kujiamini.

Kuweka malengo binafsi ni hatua nyingine muhimu katika uwekezaji wa nafsi. Malengo yanampa mtu mwelekeo na sababu ya kufanya kazi kwa bidii. Wataalamu wa maendeleo binafsi wanasema ukuaji wa kweli hutokea pale mtu anapojaribu mambo yanayomtoa nje ya eneo lake la faraja. Changamoto ndogo ndogo husaidia kukuza uwezo na kuimarisha kujiamini.

Mahusiano yenye thamani pia ni sehemu ya uwekezaji katika maisha. Marafiki, washauri na watu wanaokutia moyo wanaweza kuwa chanzo kikubwa cha maarifa na fursa. Mtandao mzuri wa mahusiano mara nyingi hufungua milango ya ushirikiano na maendeleo ya kitaaluma.

Aidha, elimu ya fedha kwa misingi ya Uislamu ni uwekezaji muhimu. Kuelewa jinsi fedha zinavyofanya kazi—kuhifadhi, kuwekeza na kutumia kwa busara—humsaidia mtu kufanya maamuzi bora katika maisha yake ya kiuchumi.

